SUPA JACKPOT
TZS. 1,152,911,993
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Samia** ateuliwa Bodi Mabadiliko ya Tabianchi duniani

UKURASA 2



TEN HAG KUAMUA HATIMA YA SANCHO

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Septemba 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581432

www.ippmedia.com


MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Wajawazito hawa hatarini vifo vya uzazi

• **Madaktari** bingwa wabainisha mzizi wa tatizo... *Endelea ukurasa 8*




## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### TUNDU LISSU ATIMKIA UBELGIJI NA MAREKANI



MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA)...

UDANGANYIFU MTIHANI

## NECTA yaonya jela miaka 20, yatoa namba kuripoti

UKURASA 2

## CHADEMA yaibua hoja nne msimamo wa Samia Katiba

UK. 3

**MICHEZO** SIMBA, YANGA ZAPEWA MAAGIZO MAZITO CAF UK.24

**KATUNI** UK.6

# Samia ateuliwa mjumbe Bodi GCA

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameteuliwa rasmi kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Kituo cha Dunia cha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCA).

Taarifa ya uteuzi huo iliwasilishwa na Ban Ki-moon, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya GCA na Katibu Mkuu mstaafu wa Umoja wa Mataifa, walipokutana kwenye Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Nairobi, Kenya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus; "Heshima hii ni utambuzi wa uongozi mahiri wa Rais Samia katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi Afrika na duniani kote, ambapo Tanzania ni kinara kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali barani Afrika."

Taarifa hiyo ilitaja wajumbe wengine wa Bodi hiyo kuwa ni Rais wa Jamhuri ya Senegal, Macky Sall, Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki Mahamat, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Akinumwi Adesina na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF), Kristalina Georgieva.

Ilisema GCA ni taasisi kubwa duniani inayosimamia masuala ya uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, hadi sasa imefanikisha upatikanaji zaidi ya Dola za Marekani bilioni 50.

Kadhalika, Tanzania ni miongoni mwa nchi za kwanza zitakazonufaika na fedha hizo katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Dk. Said Ally Mohamed, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuhusu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi unaoanza leo nchini kote. **PICHA: JUMANNE JUMA**

UDANGANYIFU WA MITIHANI

# NECTA yatahadharisha jela miaka 20, yatoa namba ya simu kuripoti hujuma

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), limetangaza namba maalum ya simu ya kuripoti udanganyifu wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la VII unaoanza leo, huku ikitahadharisha adhabu yake kisheria ni miaka 20 jela.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Said Ally Mohamed, aliwaambia jana waandishi wa habari kuwa wana uzoefu wa kushuhudia udanganyifu unaoratibiwa shuleni, ukijumuisha wanafunzi kupata majibu yanayofanana, akitaja adhabu ya awali ni kufuta matokeo.

"Shule inahusika katika kuratibu udanganyifu, unakuta darasa zima wakipata, wanapata pamoja, wakikosa, wanakosa pamoja, wakikosea herufi moja, wanakosea wote, jambo hili halivumiliki," alisema huku akitoa namba ya mawasiliano na wananchi ni 0759 360000, iwapo watahisi kuwapo na aina zozote za udanganyifu katika mtihani.

Kwa mujibu wa Dk. Mohamed aliyasema maandalizi yote yamekamilika na jumla ya masomo sita yatatahiniwa, akiyataja kuwa ni: Kiswahili, Kiingereza, Sayansi na Teknolojia, Hisabati, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi, na Uraia na Maadili.

"Maandalizi yote kwa ajili ya mtihani huo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kusambaza karatasi za mitihani na nyaraka zote muhimu," alifafanua.

Pia aliwataka wadau waache wanafunzi wafanye mitihani kwa usalama, huku akitoa takwimu za udanganyifu za kwa mwaka jana, ziliwahusu wanafunzi 2,000 kutoka vituo 25 vilivyofutwa. Mwaka juzi vituo vilivyofutwa vilikuwa vinne.

Alisema zipo shule 18,320 ambazo wanafunzi watafanya mtihani huo Tanzania Bara zikihusisha watahiniwa 1,397,370 waliosajiliwa. Kati yao, wakiwamo wasichana 742,718 sawa na asilimia 53.15 na wavulana ni 654,652 sawa na asilimia 46.85.

Dk. Mohamed alisema kati ya watahiniwa hao waliosajiliwa mwaka huu kufanya mtihani huo, 1,334,269 watafanya kwa lugha ya Kiswahili na 63,101 kwa lugha ya Kiingereza.

"Watahiniwa wenye mahitaji maalumu waliosajiliwa kufanya mtihani ni 4,583, kati yao 101 ni wasioona, 1,321 wenye uoni hafifu, 1,125 wenye uziwi, 549 ni wenye ulemavu wa akili na 1,487 ni wenye ulemavu wa viungo.

"Jumla la masomo sita yatatahiniwa ambayo ni Kiswahili, Kiingereza, Sayansi na Tenkolojia, Hisabati, Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi na Uraia na Maadili.

"Maandalizi yote kwa ajili ya mtihani huo yamekamilika ikiwa ni pamoja na kusambaza karatasi za mitihani na nyaraka zote muhimu," alisema huku akibainisha kuwa katika kukabiliana na udanganyifu hatua kubwa kwa watahiniwa ambayo huchukuliwa ni kufuta matokeo.

"Tumeshuhudia kwamba wakati mwingine udanganyifu ni unaoratibiwa na taasisi. Shule inahusika katika kuratibu udanganyifu unakuta darasa zima wakipata, wanapata pamoja, wakikosa, wanakosa pamoja, wakikosea herufi moja, wanakosea wote, jambo hili halivumiliki," alisema.

Alisisitiza kwamba watakaohusika kuhujumu mtihani, kituo husika kitafutwa kuwa kituo cha mitihani pamoja na matokeo.

**"Tumeweka mikakati nchi nzima pale ambako kuna viatarishi na kupata taarifa za siri tunachukua hatua. Niendelee kutoa onyo, tuache hawa watoto wafanye mtihani wao kwa usalama. Mwaka jana tulifuta vituo 25 pamoja na matokeo ya watahiniwa zaidi 2,000," alisisitiza.**

Dk. Mohamed alisema kwa wahusika watakaoshiriki udanganyifu huo, hatua zinazochukuliwa ni za kijinai kwa Mujibu wa sheria za Baraza ikihusisha kifungo cha miaka mitatu mpaka mitano na kwa wale ambao ni sehemu yao na kulingana na ukubwa wa kosa itatumika sheria namba 3 ya mwaka 1970 ambayo kifungo ni miaka 20.

Kuhusu matukio ya udanganyifu, alisema mwaka juzi walifuta vituo vya mitihani vinne, mwaka jana 25 na kwamba wanaendelea kuchukua hatua kuhakikisha matukio hayo yanadhibitiwa.

"Tumeweka mikakati nchi nzima pale ambako kuna viatarishi na kupata taarifa za siri tunachukua hatua. Niendelee kutoa onyo, tuache hawa watoto wafanye mtihani wao kwa usalama. Mwaka jana tulifuta vituo 25 pamoja na matokeo ya watahiniwa zaidi 2,000," alisisitiza.

Alisema ziko kesi ambazo zinaendelea Shinyanga na nyingine za wizi wa mitihani katika Mahakama ya hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

"Hatua za udanganyifu hazitakuwa za kijinai peke yake bali ni pamoja na hatua za kinidhamu za utumishi wa umma. Wakifanya udanganyifu tutafuatilia na kuhakikisha mamlaka za kinidhamu zinawachukulia hatua za kiutumishi wa umma.

"Na baraza litawasimamisha kushiriki kazi maalum ya mtihani lakini itafuatilia kuhakikisha mamlaka za kinidhamu zinawachukulia hatua ikiwamo kufutwa kazi," alisema.

Kuhusu watahiniwa wenye mahitaji maalum, alisema takwimu zinaonyesha kwa mwaka huu imeongezeka kidogo.

Pia alisema idadi ya watahiniwa wanaofanya mtihani huu kwa mwaka huu ikilinganishwa na mwaka jana ambao jumla yao ilikuwa 1,350,881 imeongezeka kwa watahiniwa 13,000 sawa na asilimia 0.93.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
13.09.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumamosi tarehe **16-09-2023 hadi 19-09-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili: **T 249 EAZ / T 499 DZX T 308 EDD / T 393 DVS T 289 EDD / T 394 DVS**
2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 21.00**
   **Upana - mita 5.50**
   **Kimo - mita 4.80**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Lissu atimkia Ubelgiji, Marekani

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Bara, Tundu Lissu, ameondoka nchini juzi kupitia mpaka wa Namanga kuelekea Nairobi, nchini Kenya, ambako alianza rasmi safari ya kwenda katika mataifa ya Ubelgiji na Marekani.

Lissu, atakaa nje ya nchi kwa mapumziko ya wiki tatu, kabla ya kurudi na kuanza tena ziara katika Kanda ya Nyasa, kwa ajili ya mwendelezo wa Operesheni '+255, Katiba mpya na Okoa Bandari zetu'.

Akizungumza na Nipashe, kwa njia ya simu kuhusu kuondoka kwa Lissu nchini, Amani Golugwa, ambaye ni Katibu wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, alisema: "Mheshimiwa Lissu ameelekea Nairobi jana (juzi) anasafiri, ana safari ndefu ya Ubelgiji na Marekani.

"Tumemaliza ziara kwa hiyo, atakuwa kwenye mapumziko ya kama wiki tatu hivi ili tuweze kuanza operesheni tena.

...Kwa hiyo jana (juzi), tulimpeleka Namanga (mpaka wa Tanzania na Kenya kwa upande wa Kaskazini), anapitia Nairobi then (halafu) anasafiri kwenda nje ya nchi," alisema Golugwa, ambaye pia alikuwa Meneja Kampeni wa Lissu katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2020.

Kabla ya kuondoka nchini, Septemba 11, Lissu alihojiwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha wakiwamo viongozi wengine waandamizi wa CHADEMA, kuhusu tuhuma za kufanya mikusanyiko bila kibali na kuzuia polisi kufanya kazi yao, wilayani Ngorongoro.

Baada ya kuhojiwa kwa tuhuma hizo, alikaririwa akisema; "Lengo la kutuzuia ni ili tusiende Ngorongoro, maana wanajua tukienda Ngorongoro, kazi ya kuondoa wakazi 100,000 na ushee haitakuwa ya kawaida, lakini tunaenda kujichaji tutarudi na tutaenda kila mahali kufanya mikutano.

"Nipo nje kwa dhamana na baada ya mwezi mmoja, nitarudi polisi kama walivyohitaji na tunasubiri hatua nyingine ziendelee kama zipo."

Lissu, alikamatwa Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, majira ya saa 4:00 asubuhi, Septemba 10, mwaka huu, akiwa na viongozi wengine kwenye hotelini, wakijiandaa kwa ajili ya mkutano wa hadhara ambao ungefanyika katika viwanja wa Mazingira bora.

# CHADEMA yaibua hoja nne msimamo wa Samia Katiba

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeibuka na hoja nne kuhusu suala la muda wa miaka mitatu utakaotumika kutoa elimu kuhusu Katiba kabla ya kuendelea na mchakato wa Katiba Mpya.

Jana, ikiwa ni siku moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuweka wazi msimamo wake kuhusu mchakato wa Katiba Mpya, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, aliiambia Nipashe kuwa wanaifanyia uchambuzi hotuba ya juzi ya Rais Samia.

Katika hotuba yake, Rais Samia alisema ni lazima Watanzania waelimishwe, wajue Katiba ya nchi kabla ya kuanza mchakato wa Katiba Mpya.

Mnyika alisema watakuwa na vikao vya Kamati Kuu karibuni ambavyo pamoja na ajenda zingine, watafanya tathmini ya hali ya siasa na demokrasia nchini kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani na Uchaguzi Mkuu wa 2025 na kutoa mwelekeo kwa taifa.

"Katika hatua ya sasa, nitoe wito kwa Rais asikilize hotuba zake mwenyewe za 2021 na 2022 na 2023 za kabla ya jana (juzi) na atagundua kwamba hotuba yake ya jana haijatoa mwelekeo mwafaka kwa taifa. Kwa kutumia falsafa yake ya 4R, abadilike na kuongoza nchi kufanya 'reforms' (mabadiliko)," Mnyika alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema wanataka Rais Samia abadili mwelekeo wanaoona ni mbaya wa kutaka kutoa elimu ya Katiba kwa miaka mitatu na badala yake upelekwe bungeni muswada wa marekebisho ya sheria kuendeleza mchakato wa Katiba Mpya, ambao utaweka kisheria vyombo na ratiba ya kuanza mchakato wa katiba sasa na kuukamilisha kwa haraka.

Hoja ya pili, Mnyika alisema Rais aongoze upelekwe bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba ya Mwaka 1977 kwa maeneo ya haraka na muhimu ya kuwezesha uchaguzi huru na haki.

"Tayari CHADEMA tulishapeleka mapendekezo yetu kuhusu suala hili kupitia mazungumzo ya maridhiano kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2022 na 2023 na pia kupitia barua ya Katibu Mkuu wa CHADEMA kwa Waziri Mkuu ya mwezi Julai mwaka 2023," alisema.

Mnyika alitaja hoja ya nne ni Rais Samia abadili kauli yake ya maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kufanywa na Waziri Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mchengerwa na badala yake, aongoze serikali ipeleke bungeni muswada wa sheria katika mkutano ujao.

"Rais asitishe kupeleka bungeni muswada wanaokusudia kupeleka Oktoba 31, 2023 wa kulipa Baraza la Vyama vya Siasa mamlaka ya adhabu dhidi ya vyama kwa kile kinachoitwa self-regulation (kujiongoza) kwa kuwa una nia ovu na mbaya ya kuvitumia vyama vinavyorubunika kuadhibu vyama vinavyosimamia haki, ukweli, uadilifu, uhuru na demokrasia," alidai.

Alipotakiwa kutoa msimamo wa chama chake endapo serikali ikiendelea na hatua zake mpya, Mnyika alisema wanaamini wanayo fursa ya mwisho wa kuwasilishwa miswada hiyo bungeni. Lisipofanyika hilo, chama kiulizwe hatua zitakazofuata.

**MSIMAMO CUF**

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa Chama cha Wananchi (CUF), Mohamed Ngulangwa, alisema wao na Watanzania wanajua lini mchakato ulianza chini ya serikali ya awamu ya nne na kutolewa maoni.

"Siyo kweli kwamba mchakato ule ulihusisha wanasiasa peke yake au wanasiasa wanaohitaji 'kubaka' Katiba Mpya. Wananchi walitoa maoni yao katika maeneo yao. Mchakato ulitumia mabilioni ya shilingi, ulifanywa bila kujali ni wanasiasa au si wanasiasa," alisema.

Katibu wa Wanawake Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), Ratifa Juma, alisema muda wa kutoa elimu uliopangwa ni mrefu ingawa anaungana na Rais Samia kutoa elimu ni muhimu.

"Kuna kundi kubwa linahitaji elimu, na kutoa elimu ni suala linalohitaji muda na gharama. Kwahiyo, ninadhani ni mchakato mzuri kutoa elimu japo muda uliopangwa ni mrefu,"alisema.

Mkalimani wa Lugha ya Alama kutoka Chama Cha Viziwi Tanzania (CHAVITA), Martha Mkuchika, alisema Katiba siyo kitu kitakachopatikana kwa haraka. Kutoa elimu ni muhimu.

Mwanasiasa Mkongwe, Steven Wassira, alisema amani nchini ni suala la kihistoria. Amani hiyo inaweza ikawapo au kutoweka kutokana na kutokuwapo kwa walinzi wa amani.

Alisema amani haitegemei kuwapo taasisi kwa kuwa kuna nchi zina mahakama za juu, tume huru ya uchaguzi, lakini baada ya uchaguzi mara nyingi amani inatoweka.

***Imeandaliwa Romana Mallya na Halfani Chusi**


HELD UNDER THE PATRONAGE OF HON. DR. DOTO MASHAKA BITEKO (MP), DEPUTY PRIME MINISTER AND MINISTER FOR ENERGY, MINISTRY OF ENERGY OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

ENDORSED BY MINISTRY OF ENERGY

Tanzania Energy Congress

20 - 21 September 2023 | Dar Es Salaam, Tanzania

INVESTING IN TANZANIA'S SUSTAINABLE ENERGY ECONOMY

WITH THANKS TO OUR 2023 SPONSORS & PARTNERS TO DATE

DIAMOND SPONSOR: PANAFRICAN ENERGY an Orca Company

PLATINUM SPONSOR: equinor

SILVER SPONSORS: East African Crude Oil Pipeline, TotalEnergies

BRONZE SPONSORS: AGL, CRDB Bank, Maurel & Prom, Neway, NMB, Oryx Energies, PBZ Bank, slb

ENERGY TRANSITION PARTNER: Songas

COUNTRY PARTNER: Oman JSRS eMarketplace

KNOWLEDGE PARTNER: Hawilti

ICT PARTNER: tigo business

BRANDING PARTNER

SUPPORTING PARTNERS

ORGANISED BY dmg events

BOOK YOUR DELEGATE PASS TODAY

Contact JAYSON ESTRADA on +255755030622 or Email: info@tanzaniaenergycongress.com

tanzaniaenergycongress.com #TanzaniaEnergyCongress

217593902



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

**UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA MBARALI NA MADIWANI KATIKA KATA SITA ZA TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Jimbo la Mbarali, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Mkoani Mbeya na kata sita (6) za Tanzania Bara kuwa kutakuwa na Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Jimbo la Mbarali na Madiwani siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023. Kata zinazofanya Uchaguzi ni Nala (Dodoma CC), Mfaranyaki (Songea MC), Old Moshi Magharibi (Moshi DC), Marangu Kitowo (Rombo DC), Mtyangimbole, (Madaba DC) na Mwaniko (Misungwi DC).

1. SIKU: Wananchi watapiga kura siku ya Jumanne tarehe 19 Septemba, 2023
2. VITUO: Upigaji kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020
3. MUDA: Vituo vitafunguliwa saa 1:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 10:00 kamili Jioni

**Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi**

1. Mpiga Kura anatakiwa kwenda katika kituo alichojiandikisha na kadi yake ya mpiga kura siku ya uchaguzi.
2. Wapiga kura waliopoteza kadi zao za kupigia kura au zilizoharibika, wanaruhusiwa kutumia vitambulisho mbadala kimojawapo ya: -
   a) Hati ya kusafiria,
   b) Leseni ya Udereva, na
   c) Kitambulisho cha Taifa.

Majina yote matatu yaliyomo katika vitambulisho mbadala yafanane na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

3. Mpiga Kura akifika kituoni anatakiwa kupanga mstari.
4. Mpiga kura anatakiwa kufuata maelekezo yote atakayopewa na Karani Mwongozaji wa kituo.
5. Mpiga kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwari wapiga kura wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokuwa nao kituoni.
6. Watu wenye mahitaji maalum wanaruhusiwa kwenda kituoni na wasaidizi.
7. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili Jioni kama wapiga kura bado wapo kwenye mstari, mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wapiga kura walio kwenye mstari watakapomalizika. Mpiga kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupiga kura.
8. Baada ya kumaliza kupiga kura, mpiga kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupigia kura.

Kumbuka kupiga kura ni haki yako ya msingi jitokeze siku ya uchaguzi ukamchague Mbunge na Diwani unayemtaka siku ya Jumanne,tarehe 19 Septemba, 2023.

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

217578702

# Lugha alama, elimu jumuishi kuwa masomo ya lazima kwa walimu wote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema somo la elimu jumuishi na lugha ya alama litakuwa la lazima kwa mtu yeyote anayeandaliwa kuwa mwalimu nchini.

Akizindua jana miongozo minne ya elimu maalum na jumuishi jijini hapa, Prof. Mkenda alisema katika Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 toleo la 2023, serikali itahakikisha kunakuwa na mazingira wezeshi ya utoaji wa elimu na mafunzo jumuishi katika ngazi zote za elimu.

"Suala la lugha ya alama na alama mguso yataimarishwa katika ufundishaji wake na somo la elimu jumuishi na lugha ya alama yatakuwa masomo ya lazima kwa walimu tarajali wote kwenye vyuo vya ualimu ili kila mwalimu afundishe kwa ufasaha darasani katika shule jumuishi.

"Tunahamasisha elimu jumuishi huwezi kuwa na walimu ambao hawawezi kufundisha kwa namna ambayo inawafikia wanafunzi wote, hili somo la elimu jumuishi na lugha ya alama kwenye rasimu ya sera litakuwa ni lazima kwa mtu yeyote anayeandaliwa kuwa mwalimu hapa nchini,"alisema.

Alitaja miongozo minne iliyozinduliwa kuwa ni mwongozo wa shule ya nyumbani, ziara ya nyumbani, upimaji na ubainishaji na uendeshaji wa elimu maalum na jumuishi.

"Miongozo hii italeta mabadiliko chanya miongoni mwa wadau katika kutimiza azma ya serikali ya kuwapatia fursa ya elimu bora wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini," alisema.

Alitoa rai kwa viongozi, wakuu wa taasisi na wadau wanaojishughulisha na utoaji elimu maalum na jumuishi kuendelea kushirikiana na serikali kuhamasisha umuhimu wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.

"Natoa rai kwa familia na wadau wa maendeleo waendelee kuona umuhimu wa kuchangia juhudi za serikali katika kuwapatia huduma stahiki wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa ujifunzaji,"alisema.

Alihimiza wazazi kuona umuhimu wa kuandikisha watoto wote wenye mahitaji maalum katika shule kwa kuzingatia mahitaji ya mtoto.

"Kwa wale watakaohitaji huduma hii ipelekwe majumbani basi wawasiliane na sisi ili kuangalia namna tutakavyoweza kufikisha huduma hii nyumbani kwa mtoto,"alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Elimu Maalum wa Wizara hiyo, Dk.Magreth Matonya alisema miongozo hiyo inakwenda kuboresha utoaji wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum.

"Huu mwongozo wa shule ya nyumbani tumekuwa tukiusubiri sana tumekuwa na changamoto kwamba tuna watoto wengine hawawezi kukaa darasani kwa ajili ya changamoto za afya na ulemavu wa kiwango cha juu wapo majumbani, tukakaa tukasema tuanzishe ambao utasaidia kuhakikisha kwamba hatuwaachi nyuma kwenye upataji elimu.

"Ni mwongozo ambao unasaidia kuwafuata watoto wenye changamoto hizi majumbani na kuwafundisha. wana namba za usajili na mitihani yote wanafanya nyumbani na masomo yote ambayo wenzao wa darasa husika kwenye shule za kawaida wanasoma Ali Kimara yupo Shule ya Msingi Diamond, alisema.

Alisema mwongozo wa ziara ya nyumbani unakwenda kuwasaidia walimu wanaokwenda ziara za nyumbani kupata taarifa zitakazowezesha kuchukua hatua stahiki.

Mkurugenzi wa Elimu kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Susan Nussu, alisema katika sensa waliyoifanya ya watoto wenye mahitaji maalum hadi Machi mwaka jana walikuwa 66,000 na zaidi ya 55,000 wako shule za msingi na wengine waliobaki wapo sekondari.

Naye Mzazi wa Ali Kimara ambaye mtoto mwenye ugonjwa adimu, Sharifa Mbarak, alisema miongozo hiyo ni moja ya hatua kubwa zilizopigwa na taifa katika utoaji elimu stahiki kwa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

# Mbarawa akerwa kasi uendeshaji wa TRC

**Na Pilly Kigome**

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema haridhishwi na kasi ya uendeshwaji wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), kwa kuwa limeshindwa kufikia malengo yaliyowekwa.

Prof. Mbarawa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa bodi mpya ya shirika hilo.

Alisema TRC ingawa linafanya kazi kubwa kwenye ujenzi wa miundombinu, katika uendeshaji wa reli halifanyi vizuri.

"Mmeshindwa kufikia malengo tuliyoweka. Kuna mikataba inawekwa baina ya bodi na wizara lakini bado malengo hayafikiwi. Hata kama mtendaji mkuu ukiniangalia huu ndio ukweli na utabaki kuwa ukweli.

"Shirika kubwa kama la TRC ipo tiketi mtandao lakini inasuasua inakuwaje, kwenye oparesheni TRC hatufanyi vizuri huu ndio ukweli ndugu zangu," alisema Mbarawa.

Pia alisema Kigoma kuna watu wamelipa kusafirishiwa saruji yao lakini hakuna hata shehena inayokwenda na kwamba pamoja na kupiga simu hakuna kinachofanyika, jambo linaloonekana dhahiri kwamba shirika halifanyi vizuri.

"Tulitegemea saruji iwe bei rahisi lakini unakwenda Kigoma mkandarasi anakwambia kazi imesimama hajapata saruji. Sasa moja ya kazi yenu bodi ni hii, ningetamani hili mliangalie," alisisitiza.

Mbarawa pia aliliagiza shirika hilo kujipanga katika uendeshaji wa Reli ya Kisasa (SGR) kwa kuwa tayari serikali imepitisha sheria kuruhusu sekta binafsi kutumia reli.

"Serikali imewekeza fedha nyingi ujenzi wa SGR. Tusipokuwa waangalifu kwa siku zitapita treni tatu tu. Tunataka kuona reli inakuwa 'active', kila kampuni ambayo itakuwa na mabehewa yake inaweza kupitisha." alisema.

Alibainisha kuwa haitakiwi kuona mtu ana mzigo wake Kigoma anasubiri TRC na kusisitiza kuwa duniani reli hazisimami bali zinafanya kazi usiku na mchana, hivyo wajiandae kushirikisha watu binafsi katika usafirishaji wa mizigo kupitia reli.

Kuhusu changamoto za shirika hilo alisema tayari serikali imetenga fedha kulipa madai mbalimbali ya wafanyakazi na kuwataka kuendelea kuwa watulivu.

Aidha, Mbarawa aliliruhusu shirika hilo kutangaza nafasi za ajira kukidhi mahitaji ya wataalam lakini akatahadharisha kuepuka upendeleo na undugu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya RTC, Ally Karavina, alimhakikishia Waziri Mbarawa kuwa watafanya maboresho ya uendeshaji wa shirika ili kufikia malengo yaliyowekwa.


## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD, AMA'Z AUCTION MART & GERERAL BROKER LTD na HARVESTER CAPITAL INVESTMENT LTD** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) au Siku Saba (7) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GAIMO CONSTRUCTION COMPANY LIMITED | GAUDENCE VICENT LYIMO AND MONICA GAUDENCE LYIMO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI Na.21393, PLOT Na.407, BLOCK 'JJ' | OLOIRIEN, MANISPAA YA ARUSHA | 29/09/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | HARVESTER CAPITAL INVESTMENT LTD |
| 2 | ZACHARIA ROMAN DAUDI | ZACHARIA ROMAN DAUDI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI YA KIMILA Na.42BGM/2845 | KIHANGAIKO, MANISPAA YA CHALINZE, PWANI | 30/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 3 | ZACHARIA ROMAN DAUDI | ZACHARIA ROMAN DAUDI | NYUMBA NYENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MSATA, WILAYA YA CHALINZE, PWANI | 30/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 4 | ZACHARIA ROMAN DAUDI | SUZANA ABELI MWELEKA | NYUMBA NYENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MSATA, WILAYA YA CHALINZE, PWANI | 30/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 5 | MATINDE T. MENDO & BOSCO G. NDUNGURU T/A LAURA SOAP | BOSCO G. NDUNGURU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO SERIKALI YA MTAA | MSINGWA, BONYOKWA, MANISPAA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 29/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 6 | WILFRED MICHAEL BATAKANWA | YUSTA MICHAEL BATAKANWA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI No.155493 PLOT NO 919, BLOCK "B" | KIZINGA, MANISPAA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 02/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD |
| 7 | PAUL J. MUHIRI | PAUL JULIAS WANGUBO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.ILA029742 | KIPUNGUNI B, KITUNDA,MANISPAA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 30/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GERERAL BROKER LTD |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| | | |
|---|---|---|
| **AMA'Z AUCTION MART & GERERAL BROKER LTD P.O. Box 62163**<br>**Dar es Salaam**<br>**Tel: 0658 100 737/ 0678 220 068**<br>**Email: amazauctionma@gmail.com** | **MANGWEMBE 2011 COMPANY LTD**<br>**P.O.Box 12943**<br>**Arusha**<br>**Tel: 0752 632 033/ 0628512033**<br>**Email:** mangwembe@gmail.com | **HARVESTER CAPITAL INVESTMENT**<br>**P.o.Box 11898**<br>**ARUSHA**<br>**Tel: 0784 200283/ 0767529605**<br>**Email: harvestercapital558@gmail.com** |

217597102

# Hoja tano zaibuliwa ziara Pemba Katibu Mkuu ACT

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KATIBU Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu, amehitimisha ziara yake kisiwani Pemba, wananchi wakiibua mambo matano wanayotaka hatua zichukuliwe.

Katika ziara hiyo iliyoanza Septemba 9 mwaka huu, Ado alishiriki kama mgeni rasmi mikutano mikuu ya majimbo ya Mtambwe, Wingwi, Kiwani na Wawi.

Katibu Mkuu alishiriki pia shughuli mbalimbali za kijamii kama vile fainali ya ligi iliyoandaliwa na Mbunge wa Wete, Omar Ali Omar na kuwajulia hali wagonjwa, yatima na vizuka.

Katika ziara hiyo, masuala makuu matano yaliibuliwa kutokana na hotuba na maelekezo ya Katibu Mkuu kwa wajumbe wa mikutano mikuu, yakijumuisha chama kuendeshwa na wanachama.

Katibu Mkuu alisema chama kimeanzisha mfumo wa kusajili wanachama wa ACT Kiganjani ili pamoja na mambo mengine, kuwezesha chama kuendeshwa na wanachama kupitia malipo ya ada za uanachama.

Hoja ya pili kwa mujibu wa Ado ni kuyarejesha majimbo yote 18 ya Pemba waliyoyapoteza katika uchaguzi uliopita.

"Majimbo mengi yamesajili wanachama zaidi ya nusu ya wapigakura wote wa majimbo husika. Hii ni ishara kuwa majimbo haya yote 18 ni ya ACT Wazalendo. 2025 tutahakikisha tunayarejesha majimbo yote mikononi mwetu" alisema.

Katibu Mkuu Ado pia aliwapongeza viongozi wa majimbo na mikoa ya Zanzibar kuhakikisha uchaguzi wa matawi unakwenda vizuri kwa upande wa Unguja na Pemba.



Jambo la nne ni kile alichokiita Ado kuwa ni kupigania mamlaka kamili ya Zanzibar, akisema: "Wazanzibari wanajua wanachokitaka. Hakijawahi kubadilika tangu enzi za chama kimoja hadi enzi za vyama vingi."

Jambo la tano kwa mujibu wa kiongozi huyo ni mageuzi ya kisiasa Zanzibar, akisema chama kina imani na mazungumzo ya maridhiano yanayoendelea baina ya ACT Wazalendo na CCM chini ya uenyekiti wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman.

Alisema ni imani ya chama kuwa mazungumzo hayo yatahakikisha kuwa makubaliano baina ya Maalim Seif Sharif Hamad na Rais Hussein Mwinyi kabla ya ACT Wazalendo kujiunga na Serikali ya Umoja wa Kitaifa yatazingatiwa ili uchaguzi ujao wa Zanzibar uwe wa haki, wazi na huru.

Ziara hii ya Katibu Mkuu Kisiwani Pemba ni mwendelezo wa ziara yake ya kutembelea mikoa mbalimbali kufuatilia maendeleo ya uchaguzi wa ndani. Kabla ya kutembelea Pemba, katika kipindi cha miezi miwili iliyopita, Katibu Mkuu Ado alishatembelea mikoa ya Kigoma, Tabora, Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Mkoa wa Kichama wa Selous na Ruvuma.

# Vijana 200 wajengewa uwezo kilimo nyumba

**Mwandishi wetu,** GEITA

KATIKA kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, shirika lisilo la kiserikali la Kijani Consalt limewajengea uwezo vijana 200 wa wilaya ya Geita, ili walime kilimo cha mboga kinachokabiliana na ukame kwa kutumia kitalu nyumba.

Vijana hao wanajengewa uwezo kupitia mradi wa Nanenane unaotekelezwa katika kata tano za wilaya hiyo kwa gharama ya Sh. milioni 200 na tayari vijana 25 kati yao wamepewa mafunzo ya uongozi ili wahamasishe vijana wenzao kujiunga katika kilimo kwa kuwa na mashamba darasa ya mfano yaliyotengenezwa kwenye maeneo yao.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Mandolin Kahindi, alisema walengwa wamepewa mafunzo ya kujua mabadiliko ya tabianchi, athari zake na njia sahihi za kukabiliana nazo.

"Tumetekeleza mradi utakaowezesha vijana kufanya kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi, ili waweze kujipatia maendeleo. Lengo ni kuwezesha vijana kunufaika na kilimo wakati huu tunaokabiliana na mabadiliko ya tabianchi,"alisema.

Kahindi alisema kilimo kimekuwa na changamoto nyingi zinazowafanya vijana wakate tamaa kwa kuwa wanalima kwa muda mrefu na mwisho wa siku wanapata hasara, lakini kupitia kilimo kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi kitakuwa na manufaa kwao na kuwakwamua kiuchumi.

Baadhi ya wanufaika wa kilimo cha kitalu nyumba, wakiwamo Davitha James na Musa Yohana wanaofanya shughuli zao katika kata ya Ihanamilo, walisema kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia kitalu nyumba mbali na kuwaondoa kwenye kilimo cha kubahatisha, kitawasaidia kupata mazao mengi na kujikwamua kiuchumi.

"Hapa tunalima nyanya ndefu, ukilima nje hazihimili misukosuko kama mvua nyingi, upepo na jua kali. Aina hii ya nyanya inadumu muda mrefu, ndani ya miezi sita hadi nane. Ukiwa unachuma kwa kutumia kitalu nyumba, mazao yako yanakuwa hayana viuatilifu tofauti na kulima nje, unatumia viuatilifu vingi kuua wadudu, lakini pia mazao ni machache maana ni kilimo cha muda mfupi," alisema James.

Bahati Lubinza na Matrida Filipo, walisema kilimo cha kutumia kitalu nyumba kinawasaidia kulima wakati wote - uwe wa mvua au jua bila kuwa na hofu ya mazao kuathiriwa na ukame au mvua nyingi.

Ofisa Ugani Kata ya Nyanguku, Juma Hamad, akizungumzia mradi wa kitalu nyumba, alisema kilimo hicho ni suluhisho la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kuwa utawezesha vijana kuzalisha kwa mwaka mzima na kujiongezea kipato.

Ofisa kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Maliki Athumani, alisema halmashauri hiyo imekuwa inatumia fungu la mikopo kwa vijana kuwekeza kwenye kilimo na kila kata wametengeneza mashamba darasa ambayo vijana wanajifunza namna ya kulima kilimo bora kitakachowanufaisha.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi Kilindi wameonesha njia, wengine waige

**MARA** kwa mara wananchi wanapotaka maendeleo ya jambo lolote ni lazima kilio chao kiende serikalini kwa sababu wanajua ndio kimbilio lao la utatuzi wa kero zao.

Linapokuja suala la maendeleo ya barabara, ujenzi wa vituo vya afya au shule, kilio hupelekwa serikalini wakijua kuwa kodi wanazochangia katika maeneo mbalimbali zifanye kazi hiyo.

Lakini kwa wakazi wa vitongoji vya Losiai, Luhondo Mafisa na Kijiji cha Makelele, Kata ya Pagwi Wilaya ya Kilindi, haikuwa hivyo, waliamua kujenga shule kwa njia ya kujitolea ili kulinda maisha ya watoto wao waliokuwa wanalazimika kuvuka mto kufuata shule kwenye kijiji kingine umbali wa kilometa saba.

Wangekuwa wananchi wengine wasiokuwa na ushirikiano, wangeamua kusubiri serikali mpaka ipange bajeti yake ya kujenga shule hiyo huku watoto wakiendelea kuteseka.

Wananchi hao waliamua kufanya harambee ya ujenzi wa shule hiyo inayojengwa katika kitongoji cha Losiai, kutokana na hatari waliyokuwa wakipitia watoto wao kuvuka mito mikubwa na mapori.

Kwa hiari yao wameamua kujenga shule hiyo na wanatarajia kuomba kupata usajili ili kuwa shule kamili baada ya kukamilika ujenzi na wanachoiomba serikali ni kuwaunga mkono katika suala hilo.

Wananchi hao wameonesha mfano wa kuigwa kwa juhudi zao za kuhakikisha watoto wao wanakuwa salama kwa kusoma mahala pazuri na kuwaepusha na hatari walizokuwa wakikabiliana nazo njiani wakati wa kwenda shule.

Watu wengi hupenda kuchangia sherehe za harusi na mambo mengine ya starehe, lakini linapokuja suala la maendeleo wanakuwa wagumu na badala yake wanasubiri serikali iwafanyie.

Wakati mwingine hata barabara za mitaani wanamoishi ziko katika hali mbaya, lakini baadhi ya wananchi wanagoma kujitolea kuchangia kujaza hata vifusi ili ziweze kupitika vizuri, wakisubiri serikali ifanye kazi hiyo.

Barabara hizo ndizo zinategemewa kama kukitokea tatizo la janga la moto magari yaweze kupita vizuri na kuzima moto. Lakini kwa sababu ya kutoonesha utayari wa kujitolea nyumba zinazopata majanga kama hayo huishia kuteketea kwa sababu ya gari la zimamoto kushindwa kufika sehemu husika kutokana na kukosa njia ya kupita.

Vile vile, wagonjwa wengine hawawezi kufika hospitalini kwa sababu ya kushindwa kutoka nyumbani kutembea hadi vituo vya mabasi ya umma, wanahitaji kufuatwa na gari, lakini kwa kuwa hakuna njia, anaweza asipate huduma na kupoteza maisha.

Juhudi zilizooneshwa na wananchi walioamua kujenga shule kwa kujitolea ni mfano tosha kuwa sio kila jambo lisubiri serikali, tukianza kuonesha juhudi zetu wenyewe ni rahisi kwa serikali kuunga mkono kwa kutoa msaada zaidi.

Ni mambo mangapi yanakwama kwa sababu tu wananchi wameshindwa kuonesha ushirikiano na umoja wa kuamua kutekeleza jambo fulani na matokeo yake watu wote kuathirika kama hawajatokea wachache wenye moyo wa maendeleo kutekeleza.

Wewe mwananchi ni lazima ujiulize kama sio wewe kuonesha uzalendo, unataka mtu wa nje ndio aje kukufanyia maendeleo?

Mambo mengine ni lazima wananchi waoneshe kujitoa ili juhudi zao ziweze kuungwa mkono.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Mliovurunda vibao makazi mgharamie

**LICHA** ya serikali kutekeleza mpango wa kuweka vibao vya namba za nyumba na majina ya mitaa katika maeneo mbalimbali nchini, ili kutambulisha makazi mijini na vijijini kuna wasiwasi kuwa pengine mambo hayajakaa sawa.

Kazi hiyo iliyofanyika kwa miaka kadhaa sasa ya kuwa na mfumo wa anuani za makazi baada ya waliopewa jukumu la kufanya kazi hiyo kupita kwenye mitaa mbalimbali kuorodhesha idadi ya nyumba, mitaa na barabara.

Zoezi hilo lilifanyika kwa weledi na baadhi ya nyumba kupata namba na hata majina ya mitaa na barabara kulingana na makubaliano ya baadhi ya wakazi au matakwa ya mtu mmoja mmoja, aliyeruhusiwa kulipia na kutumia jina alilolitaka.

Pamoja na mafanikio hayo, kuna taarifa za kuwepo dosari zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa mparanganyiko wa namba kutokana na kukosekana kwa mpangilio unaoeleweka wa wakati wa kuzibandika katika baadhi ya nyumba na mitaa.

Miongoni mwa maeneo jijini Dar es Salaam yanahusika na kuzua sintofahamu kwa watendaji wa mitaa hiyo ambao wamekuwa wakiulizwa mara kwa mara na wananchi.

Kwa mfano namba katika mtaa zinatakiwa kuwa na mpangilio unaoanzia na 1, 2,3, 4 na kuendelea, lakini cha kushangaza ni kwamba, namba inayoanza inasomeka mwanzoni mwa mtaa, ikifuatiwa na ya pili, badala ya tatu na kwa mfuatano huo.

Kisha utakuta kuna namba inayofuatia isiyokuwa katika mpangilio unaoeleweka kana kwamba imechomekwa, hivyo kusababisha usumbufu endapo mlengwa anaweza kuwa na mahitaji ya kupata huduma muhimu kama usafiri , tiba na kupambana na ajali ya moto.

Wengi, waliopewa utambulisho wameonyesha kutoridhishwa na katika vikao vyao vya maendeleo, wamekuwa wakihoji sababu ya dosari hiyo kujitokeza na kutaka kufanyiwa marekebisho.

Pamoja na baadhi ya watendaji kujitetea kuwa dosari hizo zitafanyiwa marekebisho, maswali ya kujiuliza ni kwamba gharama zitakuwa ni za nani, ikikumbukwa kwamba kila mkazi aliyefikiwa na zoezi hilo alilipa Shilingi 10,000 kwa ajili ya kulipia namba na kubandika kwenye nyumba yake.

Ni ukweli usiopingika kwamba zoezi hilo ambalo lilinasimamiwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) lina manufaa kwa jamii, kwa kuwa litarahisisha kufikisha huduma muhimu za jamii na kuondoa usumbufu kwa kutumia muda mrefu kutafuta nyumba lakini kasoro inayoripotiwa inakwamisha.

Kinachoonekana hapo, vijana waliopewa kazi hiyo, waliifanya kufunika kombe mwanaharamu apite, bila kuzingatia mpangilio na maelekezo.

Inawezekana walifanya hivyo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kuwakosa wenye makazi kwa kuwa wangewapa ushirikiano, hivyo kuorodhesha nyumba kwa kuziruka nyingine, kisha kurudia na kusahau kuweka namba katika mpangilio unaotakiwa na kuzua malalamiko na sintofahamu hiyo kati ya wananchi na viongozi wao.

Kingine kinachoonekana hapo, ni baadhi ya vijana waliopewa kazi ya kuhesabu nyumba hizo ni kutokuwa na elimu ya kutosha.

Lakini, kabla ya kuanza kwa zoezi hilo, viongozi wa mitaa husika, walitakiwa kujiridhisha kwanza elimu ya vijana hao waliopewa dhamana hiyo, endapo ingebainika kuwepo na mapungu, wangepigwa msasa badala ya kujitetea kuwa walijiongeza.

Ikumbukwe pia , mbali na wananchi kulalamikia gharama kwa ajili ya kupata vibao hivyo, pia serikali inatumia fedha nyingi kwa kufanikisha zoezi hilo ambalo haijajulikana litakamilika lini, japo kumekuwa na taarifa kuwa limesimama huku wananchi wakitakiwa kujitokeza kuchukua vibao vya namba zao na kwenda kuzibandika kwenye makazi yao.

Wajumbe nao wanatakiwa kujua kuwa wana dhamana ya kupitia kwenye maeneo yao kufuatilia ubandikaji wa namba hizo ili kuondoa dosari hizo badala ya kusubiri wananchi au kuwachochea kwenda kulalamika kwenye mikutano na viongozi wao wa serikali za mitaa kwani wao ndio walioko karibu nao zaidi.

HABARI KITAIFA

# NEMC yapokea malalamiko 230 kelele baa na kumbi za starehe

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa na Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele umeanza upya na wamepokea malalamiko zaidi ya 230.

NEMC imewaonya wamiliki wa baa, kumbi za starehe na burudani kwamba haitasita kufunga biashara zao iwapo wataendelea na tabia hiyo.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam jana na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la uchafuzi wa mazingira kwa kelele zilizopita viwango licha ya baraza hilo kutoa elimu kwa umma na wamiliki wa kumbi hizo na baa.

"Tuliokuwa tumewafungia walitii wakatimiza masharti tuliyowapa tukawafungulia, lakini ndani ya mezi mitatu tumepata malalamiko zaidi ya 230 ya kelele kwa hiyo tunawaonya waachane na kelele kabla hatujaanza kuchukua hatua kali kama zilizopita," alisema.

Alisema wote waliokuwa wamefungiwa walifunguliwa na kuendelea na biashara zao kama kawaida, lakini katika siku za karibuni wamejisahau baada ya kuona utulivu na wameanza tena kupiga kelele hizo.

"Juzi juzi kiongozi mmoja wa kitaifa alinipigia simu usiku akisema kwamba ameshindwa kulala yeye na familia yake kwasababu kuna baa jirani yake inapiga muziki kwa sauti kubwa sana kwa hiyo tutachukua hatua," alisema.

Dk. Gwamaka aliwakumbusha wamiliki hao kuwa sheria bado ipo na inafanyakazi na NEMC itaendelea kuwaelimisha kwamba kelele ni uchafuzi, lakini wale watakaokaidi haitasita kuwachukulia hatua kama za hivi karibuni.

"Uchafuzi unapofanywa saa nne baada ya watu kulala unasababisha athari kubwa sana kwa sababu kama watoto wanakosa usingizi mzuri hivyo wanashindwa kuamka kwenda shule kwa wakati, kuna wagonjwa na watu wazima ambao wanahitaji utulivu," alisema

"Si kwamba NEMC inaona sifa kufunga biashara ya mtu, tunajua biashara hizo zimeajiri watu wengi sana na zinalipa kodi, lakini kelele nazo zimekuwa zikisababisha athari kubwa kwa wananchi kwa hiyo fanya biashara yako bila kuathiri maisha ya mtu mwingine," alisema.

Mei, mwaka huu NEMC iliendesha operesheni ya kufungia nyumba za starehe na baa kutokana na kukiuka masharti ya leseni zao na kupiga kelele zilizovuka kiwango kinachokubalika kisheria.

Kwenye operesheni hiyo ya Mei, Dk. Gwamaka alisema baa zilizofungwa Wilaya ya Kinondoni zilikuwa 19, Ilala 25, Kigamboni 22, Temeke 12, Dodoma, tano na Mwanza sita na kwamba walianzia maeneo hayo kutokana na kuwa na malalamiko mengi.

Alisema wenye kumbi za starehe na baa ambazo wamekuwa wakirudia kufanya makosa hayo watatozwa faini ya Sh. 5,000,000 ambayo watapaswa kuilipa ndani ya siku 14.

Alisema wakosaji wa mara ya kwanza watatakiwa kulipa faini ya Sh. 2,000,000 ndani ya siku hizo 14 na kwamba wote watafunguliwa kuendelea na biashara zao iwapo watafuata masharti yaliyowekwa na baraza.

# Walimu wapya wapewa somo la maadili kazini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WALIMU wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, wametakiwa kuzingatia maadili na kuepukana na matumizi ya dawa ya kulevya, unywaji wa pombe kupindukia ili watimize wajibu wao wa kuboresha taaluma na ufaulu kwa wanafunzi.

Kauli hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Wilaya ya Morogoro, Mbaruku Chipeta, wakati akizungumza na walimu wa ajira mpya walipangiwa vituo vya kazi katika shule mbalimbali za msingi na sekondari wilayani humo.

Chipeta alisema mwalimu ni kioo kwa jamii inayomzunguka na maadili yake yanatoa taswira chanya kwa wanafunzi anaowafundisha na kwa kuwa haiba yake inamwongezea ari mwanafunzi kufuata nyayo na maadili mema kwa maisha yake kielimu na kijamii.

Alisema kuwa chama cha walimu kina jukumu la kuwatetea walimu kote nchini kwa kuweka mshikamano kwa kuzingatia kauli mbio yao wajibu na haki, hivyo mwalimu anapotimiza wajibu wake anapaswa kutetewa kupata haki yake ikiwamo masilahi na kulipwa stahiki zake kwa wakati.

"Niwaombe walimu wenzangu mliopata ajira hii mpya, mkalete chachu kwenye kuleta mapinduzi ya kuboresha elimu kwa kuwa hali ya ufaulu kwa shule zetu katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni siyo ya kuridhisha, tushirikiane katika kuboresha ufaulu katika shule zetu," alisema.

Aidha, alitoa rai kwa walimu kuepukana na kuchukua mikopo kwenye taasisi zisizo rasmi na badala yake watumie taasisi rasmi za fedha ikiwamo kwenye benki ambako ni salama zaidi.

Naye Ofisa Utumishi Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, B'hango Lyangwa, aliwataka walimu hao kuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, katika utendaji kazi kwa uweledi ili kuleta ufanisi kwenye sekta ya elimu.

Lyangwa alisema, jukumu la walimu kote nchini ni kuhakikisha taifa linaondokana na adui ujinga, utendaji wa kazi wa mwalimu ndiyo unaofinyanga wanajamii kwa kutoa maarifa mbalimbali yanayosaidia kujenga taifa.

Aliwakumbusha walimu hao kutojihusisha na makundi yasiyo kuwa na maadili watakayokutana nayo katika jamii.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA NISHATI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

ewura

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu na 19(2)(a) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni kutoka kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira kwa ajili ya kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira. Maelezo ya Waombaji ni kama yalivyotolewa hapa chini:-

| S/No | Mwombaji | Anwani | Chanzo cha Maji | Miundombinu | Maelezo ya Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Busega | S.L.P 494 Bariadi. Barua pepe: info@busewasa.go.tz | Ziwa Victoria kutoka katika mabanio matatu yaliyoko maeneo ya Mwabulugu, Bulima na Lukungu yenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 5496 kwa siku | Matenki ya maji saba yenye uwezo wa jumla ya mita za ujazo 1085. Mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilometa 224.14 pamoja na vilula 100 | Leseni ya kutoa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika vijiji vya Lamadi, Mwabayanda ,Kalago, Lukungu, Mkula na Nyashimo |
| 2. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Rombo | S.L.P 244, Rombo Mkuu. Tanzania. Barua Pepe: md@rombowssa.go.tz | Vyanzo thelathini (30) vya mto na chemchem na vyanzo vya chini ya ardhi vinajumuisha visima virefu sita (6). Jumla ya uwezo wa kuzalisha maji kwa vyanzo vyote ni mita za ujazo 21,445 kwa siku | matenki ya maji mia moja na kumi na mbili (112) yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 11,999.5. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 956, pamoja na vilula vinavyofanya kazi mia mbili tisini na sita (296) | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Wilaya ya Rombo |
| 3. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe | S.L.P 81, Njombe. Tanzania. Barua Pepe: info@njuwasa.go.tz | Mamlaka inapata maji kutoka kwenye vyanzo vitano(5) vya chemchem. Jumla ya uwezo wa kuzalisha maji kwa vyanzo vyote ni mita za ujazo 7,278.8 kwa siku | Mamlaka ina matenki ya maji kumi na sita(16) yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 1,270. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 188.4 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Njombe |
| 4. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela - Kasumulu | S.L.P 237, Kyela. Tanzania. Barua Pepe: mdkyelakasumulu@maji.go.tz | Mamlaka inapata maji kutoka kwenye vyanzo viwili(2) vya mto na visima virefu vinne(4). Jumla ya uwezo wa kuzalisha maji kwa vyanzo vyote ni mita za ujazo 8,896 kwa siku. | Mamlaka ina matenki ya maji kumi na moja(11) yenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha mita za ujazo 1,170. Muombaji pia ana mtandao wa majisafi wenye urefu wa kilomita 61 | Leseni ya kutoa huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji ya Kyela na Kasumulu. |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana dhidi ya maombi tajwa hapo juu, awasilishe kwa maandishi EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia siku ya kuchapishwa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu yeyote kwa maombi maalum ya maandishi.

**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi**
**S. L. P 2857, Dodoma.**
**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz**
**Tovuti: http./www.ewura.go.tz**

217595502

Jengo la EWURA, Kiwanja Na 3, Kitalu AD, Medeli Magharibi, S.L.P. 2857, Dodoma, Simu: +255 26 2329003-3, Nukushi: +255 26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz • Tovuti: http://www.ewura.go.tz



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Lindi, Twaiba Mpako (wa pili kushoto) na viongozi wenzake wakiwapa zawadi ya watoto wanaosoma shule ya awali Rutamba, Jimbo la Mchinga mkoani humo, wakati Kamati ya Utekelezaji ya UVCCM ilipofanya ziara kituoni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makundi hatarishi vifo vya uzazi yaanikwa

## •Mwaka 2022/23, vifo 943 vilitokea nchini

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2022/23, kulikuwa na vifo 943 vitokanavyo na uzazi nchini kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Wataalamu wabobezi katika afya ya uzazi wameyataja makundi ya wajawazito walio hatarini zaidi kupoteza maisha wakati wa kujifungua, yakijumuisha wenye unene uliopitiliza na wanaojifungua kwa njia ya upasuaji.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Lilian Mnabwiru, alibainisha makundi hayo juzi wakati wa semina iliyofanyika Kinondoni, mkoani Dar es Salaam kwa lengo la kuwaleta pamoja wataalamu wa afya ya uzazi na waandishi wa habari.

Dk. Lilian aliyataja makundi mengine ni ya wajawazito ambao kondo liko sehemu isiyo sahihi; kondo kutangulia kabla ya mtoto; kondo kupasuka kabla ya mtoto kuzaliwa na kondo kuchukua eneo kubwa zaidi katika kuta za uzazi.

Kwa mujibu wa bingwa huyo, makundi mengine ya wajawazito wanaoongezwa njia au kuwekewa vifaa maalum vya kupanua njia; kujifungua; waliowahi kufanyika upasuaji; kuwahi kubeba ujauzito baada ya kufanyiwa upasuaji; wenye uzazi pingamizi na watoto wanaotanguliza makalio.

"Wanawake wanne sana; wenye uzazi pingamizi; wenye ujauzito wa pacha; wenye upungufu wa damu; kasoro katika mfumo wa kugandisha damu na watoto waliofia tumboni, wako hatarini kupoteza maisha wakati wa kujifungua," alisema.

Bingwa huyo alisema kukabiliana na shida hizo, ni muhimu watalaamu wa afya kuboresha mbinu za kutibu wagonjwa kulingana na mabadiliko ya teknolojia.

Alisema kuwa katika kuzuia damu kutoka kwa wingi (PPH) baada ya mama kujifungua, kwa miaka mingi, wamekuwa wakitegemea matumizi ya dawa za uterasi kama vile Oxytocin, lakini katika miaka ya hivi karibuni, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilipendekeza matumizi ya Carbetocin ambayo haihimili joto na matumizi ya 'tranexamic acid' (TXA).

"Haya yanahitaji kujumuishwa katika miongozo ya kitaifa ili kuharakisha juhudi za kupunguza vifo vya uzazi," Dk. Lillian alishauri.

Katika mada yake iliyopewa jina la 'Usimamizi wa PPH: Zamani, Sasa na Wakati Ujao', Dk. Lilian aliangazia sababu kubwa za vifo vya uzazi nchini, kubwa ikiwa ni kutokwa na damu nyingi (PPH). Sababu nyingine ni maambukizi ya njia ya uzazi ya mwanamke na utoaji mimba.

Dk. Chetan Ramaiya, Makamu wa Rais wa Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Wanawake na Afya ya Uzazi Tanzania (AGOTA), alipendekeza kwamba ili vifo hivyo vidhibitiwe, hatua za sasa na miongozo ya matibabu ya kitaifa zinahitaji kuboreshwa na kubadilisha sera kwa kiasi kikubwa ili kudhibiti PPH na vihatarishi vingine.

"Kumekuwapo na maboresho makubwa katika matumizi ya teknolojia ya kidijitali na njia nyinginezo.

"Serikali imewekeza sana na kuwashirikisha wataalamu wa afya ya uzazi katika kudhibiti vifo vya uzazi. Lakini kuna nafasi ya kuboresha. Ni muhimu kwamba, kama nchi tuboreshe miongozo yetu ya matibabu ili kuendana na dawa mpya za kuokoa maisha na afua ambazo zimeonyesha ufanisi katika kupunguza vifo vya uzazi," alishauri.

Semina iliandaliwa na Shirika la Mawasiliano na Utafiti la RESEARCHCOM, ikilenga pia kujenga uwezo kwa vyombo vya habari kwenda sambamba na maendeleo ya sayansi ya matibabu juu ya afya ya uzazi.

Mnamo mwezi Mei mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy, aliliarifu Bunge kuwa wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupunguza vifo vya wajawazito.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23, vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 943 kulinganisha na vifo 982 katika kipindi kama hicho mwaka wa 2021/22.

"Hii ni sawa na kupungua kwa asilimia nne ya vifo hivi. Mikakati yetu ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma, kusogeza upatikanaji huduma za afya wakati wa ujauzito kwa kuhakikisha wajawazito wanawahi kliniki ili kupatiwa huduma stahiki kwa wakati.

"Pia kuhakikisha kuwapo dawa muhimu kwa wajawazito na upatikanaji damu salama kwa kinamama wanaohitaji kuongezwa damu, kutoa mafunzo kazini kwa mwisho kushirikiana na vyama vya kitaaluma.

"Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya wakati wa ujauzito kwa kuhakikisha elimu inatolewa kuanzia ngazi ya jamii kuhusiana na umuhimu wa mama mjamzito kuhudhuria kliniki kama inavyoainishwa katika Mwongozo wa Huduma za Kliniki kwa Wajawazito wa Mwaka 2018.

"Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, takwimu za MTUHA zinaonyesha kuwa, jumla ya wajawazito 2,028,151, sawa na asilimia 98 walihudhuria kliniki kwa mara ya kwanza, kulinganishwa na wajawazito 1,572,778 sawa na asilimia 86 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22," alisema.

Waziri Ummy aliitaja mikoa iliyoongoza kwa kuwa na asilimia kubwa ya wajawazito waliohudhuria kliniki - hudhurio la kwanza ni Katavi (asilimia 105.9), Tabora (asilimia 88.3), Geita (asilimia 78.3), Shinyanga (asilimia 77.6) na Rukwa (asilimia 76.3).

Mikoa iliyokuwa na asilimia ndogo ya wajawazito waliohudhuria kliniki - hudhurio la kwanza ni Mtwara (asilimia 43.9); Njombe, (asilimia 44.6) na Kilimanjaro (asilimia 45.8).

# Waziri Ndalichako awapa angalizo wastaafu tarajali utapeli kimtandao

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amewataka wastaafu watarajiwa kuchukua tahadhari dhidi ya utapeli, ukiwamo wa kimtandao.

Alitoa angalizo hilo juzi alipofungua semina elekezi kwa wastaafu watarajiwa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) jijini Dar es Salaam.

Prof. Ndalichako, akizungumza na wastaafu hao kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, aliipongeza PSSSF kwa kuandaa semina hiyo iliyobeba kaulimbiu ya 'Wekeza Mafao Yako Sehemu Salama kwa Uhakika wa Ukwasi'.

Alisema wastaafu wamekuwa walengwa wa matapeli, hivyo akawaasa kuwa makini na watu wanaofanya ushawishi wa kutengeneza mazingira ya kuwapo dharura.

"Mtu anapokutengenezea mazingira ya dharura, jitafakari kwanza kwanini iwe dharura. Serikali haiwezi kutaka kitu kwa dharura.

'Lipa sasa hivi'. Na unakuta mtu anatoa fedha na namba aliyopigiwa, akijaribu tena haipatikani na fedha zimekwenda," alihadharisha.

Waziri huyo alisema hiyo ndiyo sababu iliyoisukuma PSSSF kuandaa semina hiyo ili kuwajengea wastaafu wake watarajiwa uelewa na ufahamu kuhusu umuhimu wa kufanya uamuzi sahihi wa kukuza vipato vyao baada ya kustaafu ili kuleta tija na uendelevu wa kipato.

"Usia wangu kwenu ni kuyatumia vyema madini ya elimu mtakayoyapata hapa kwa kushikilia mambo makuu matatu: kuwa na mtazamo chanya, kuweka mipango makini na kutimiza ndoto binafsi baada ya kustaafu," alisema.

Prof. Ndalichako alisema kuwa kustaafu ni wajibu kwa kila mtumishi, hivyo hakuna budi kuendeleza maisha mazuri hata baada ya kustaafu.

Alisema ni vyema mtumishi akatambua kuwa safari ya kustaafu inaanza pale anapoanza ajira, hivyo ni muhimu kujiandaa kwa mipango na kifedha ili kufurahia maisha ya uhuru, lakini lazima kuwa na umakini katika usimamizi wa fedha.

"Matumizi ya busara ya fedha baada kustaafu ni muhimu zaidi kwa kuwa kwa kiasi kipato kinapungua na nguvu za kufanya kazi zinakwenda kupungua siku hadi siku," alihadharisha.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema mfuko huo unatarajia kuwa na wastaafu 11,000 kwa mwaka huu wa fedha 2023/24.

Alisema wastaafu watapatiwa mafunzo ya elimu ya uwekezaji katika masoko ya fedha, taarifa za nyaraka na utaratibu wa kufuata wakati wa kustaafu, kujiandaa kisakolojia baada ya kutoka katika utumishi, umuhimu wa kutunza mazingira wanayoishi kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uhalifu wa kimtandao ambao unaathiri wastaafu wengi.

"Mfuko katika kutambua na kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, una mpango wa kutoa mche mmoja wa mti kwa kila mstaafu wa PSSSF.

"Mpaka sasa tuna wanachama 739,000 na lengo hapa ni kila mmoja apande na kutunza mche tutakaompatia pindi atakapofikia wakati wa kustaafu," alisema Kashimba.

Semina ya aina hiyo ilifanyika mwaka 2021 kwa wastaafu watarajiwa 3700 bara na visiwani na huu pia elimu itawafikia wastaafu kwenye mikoa ya Tanzania Bara na Visiwani, alisema CPA. Kashimba.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Lindi, Twaiba Mpako (wa pili kushoto) na viongozi wenzake wakiwapa zawadi ya watoto wanaosoma shule ya awali Rutamba, Jimbo la Mchinga mkoani humo, wakati Kamati ya Utekelezaji ya UVCCM ilipofanya ziara kituoni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito hawa hatarini vifo uzazi

## ●Mwaka 2022/23, vifo 943 vilitokea nchini

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2022/23, kulikuwa na vifo 943 vitokanavyo na uzazi nchini kwa mujibu wa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

Wataalamu wabobezi katika afya ya uzazi wameyataja makundi ya wajawazito walio hatarini zaidi kupoteza maisha wakati wa kujifungua, yakijumuisha wenye unene uliopitiliza na wanaojifungua kwa njia ya upasuaji.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Lilian Mnabwiru, alibainisha makundi hayo juzi wakati wa semina iliyofanyika Kinondoni, mkoani Dar es Salaam kwa lengo la kuwaleta pamoja wataalamu wa afya ya uzazi na waandishi wa habari.

Dk. Lilian aliyataja makundi mengine ni ya wajawazito ambao kondo liko sehemu isiyo sahihi; kondo kutangulia kabla ya mtoto; kondo kupasuka kabla ya mtoto kuzaliwa na kondo kuchukua eneo kubwa zaidi katika kuta za uzazi.

Kwa mujibu wa bingwa huyo, makundi mengine ya wajawazito wanaoongezwa njia au kuwekewa vifaa maalum vya kupanua njia; kujifungua; waliowahi kufanyika upasuaji; kuwahi kubeba ujauzito baada ya kufanyiwa upasuaji; wenye uzazi pingamizi na watoto wanaotanguliza makalio.

"Wanawake wanene sana; wenye uzazi pingamizi; wenye ujauzito wa pacha; wenye upungufu wa damu; kasoro katika mfumo wa kugandisha damu na watoto waliofia tumboni, wako hatarini kupoteza maisha wakati wa kujifungua," alisema.

Bingwa huyo alisema kukabiliana na shida hizo, ni muhimu watalaamu wa afya kuboresha mbinu za kutibu wagonjwa kulingana na mabadiliko ya teknolojia.

Alisema kuwa katika kuzuia damu kutoka kwa wingi (PPH) baada ya mama kujifungua, kwa miaka mingi, wamekuwa wakitegemea matumizi ya dawa za uterasi kama vile Oxytocin, lakini katika miaka ya hivi karibuni, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilipendekeza matumizi ya Carbetocin ambayo haihimili joto na ile ya 'tranexamic acid' (TXA).

"Haya yanahitaji kujumuishwa katika miongozo ya kitaifa ili kuharakisha juhudi za kupunguza vifo vya uzazi," Dk. Lillian alishauri.

Katika mada yake iliyopewa jina la 'Usimamizi wa PPH: Zamani, Sasa na Wakati Ujao', Dk. Lilian aliangazia sababu kubwa za vifo vya uzazi nchini, kubwa ikiwa ni kutokwa na damu nyingi (PPH). Sababu nyingine ni maambukizi ya njia ya uzazi ya mwanamke na utoaji mimba.

Makamu wa Rais wa Chama cha Madaktari wa Afya ya Uzazi na Magonjwa ya Wanawake Tanzania (AGOTA), Dk. Chetan Ramaiya, alishauri kuongezwa jitihada na kuweka kipaumbele kwenye afua bunifu ili kufikia mwaka 2030 nchi iweze kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na uzazi hadi kufikia 70 kati ya vizazi hai 100,000.

Dk. Ramaiya alisisitiza afua zinazoibuka kimataifa ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kudhibiti upotevu wa damu nyingi (PPH) ambayo bado inaongoza kwa kiwango cha juu zaidi katika kusababisha idadi kubwa ya vifo vya uzazi.

"Wahudumu wa afya wanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo vya wajawazito vinavyoweza kuzuilika nchini iwapo watabadilika kulingana na mabadiliko ya kisayansi na ubunifu na mbinu bora zinazoibuliwa kimataifa katika kudhibiti vifo vitokanavyo na uzazi," alisema Dk. Ramaiya.

Rais Mteule wa AGOTA, Daktari Bingwa wa Afya ya Uzazi na Magonjwa ya Wanawake, Dk. Yahaya Kapona, alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa miaka mitano iliyopita, limependekeza kuwa dawa mpya kama vile 'Carbetocin' inayohimili joto na ile ya 'Tranexamic acid' zimegunduliwa kuwa na ufanisi katika kupunguza utokwaji damu nyingi baada ya kujifungua.

Hata hivyo, nchi nyingi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara, ikiwamo Tanzania, bado zinakabiliwa na changamoto katika kuhuisha miongozo yao ya kitaifa na orodha ya dawa muhimu ili kujumuisha dawa hizo zinazopendekezwa na WHO.

"Sasa hivi kuna dawa mpya inaitwa Carbetocin imeruhusiwa kutumika hapa nchini na kwa sasa serikali kupitia Wizara ya Afya iko mbioni kufanya mchakato wa kuiingiza katika mwongozo ili itumike katika vituo vyote vya afya nchini. Dawa hii ina faida mbili - inahimili joto na ina uwezo mkubwa wa kubana kizazi ili kuzuia damu na inatolewa mara moja tu kwa mgonjwa," alisema Dk. Kapona.

WHO ilitoa mwongozo huo baada ya kugundua kuwa juhudi za kimataifa za kukabiliana na PPH zimeshindwa kupata nguvu katika mulongo mmoja uliopita, licha ya uhitaji wa kushughulikia sababu kuu ya vifo vya uzazi.

Hali ya vifo vitokanavyo na uzazi nchini Tanzania, kwa mujibu wa Utafiti wa Demografia ya Afya (DHS) 2017, vinakadiriwa kuwa 524 kati ya vizazi hai 100,000.

Januari mwaka huu, WHO ilitoa makadirio ya takwimu ya kimataifa ya kiwango cha vifo vitokanavyo na uzazi (MMR) kwa Tanzania ni 238 kati ya vizazi hai 100,000, kiwango cha chini ni 174 kati ya vizazi hai 100,000 na kiwango cha cha juu ni 381 kati ya vizazi hai 100,000.

Semina iliandaliwa na Shirika la Mawasiliano na Utafiti la RESEARCHCOM, ikilenga pia kujenga uwezo kwa vyombo vya habari kwenda sambamba na maendeleo ya sayansi ya matibabu juu ya afya ya uzazi.

Mnamo mwezi Mei mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy, aliliarifu Bunge kuwa wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupunguza vifo vya wajawazito.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23, vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 943 kulinganisha na vifo 982 katika kipindi kama hicho mwaka wa 2021/22.

"Hii ni sawa na kupungua kwa asilimia nne ya vifo hivi. Mikakati yetu ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma, kusogeza upatikanaji huduma za afya wakati wa ujauzito kwa kuhakikisha wajawazito wanawahi kliniki ili kupatiwa huduma stahiki kwa wakati.

"Pia kuhakikisha kuwapo dawa muhimu kwa wajawazito na upatikanaji damu salama kwa kinamama wanaohitaji kuongezwa damu, kutoa mafunzo kazini kwa mwisho kushirikiana na vyama vya kitaaluma.

"Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya wakati wa ujauzito kwa kuhakikisha elimu inatolewa kuanzia ngazi ya jamii kuhusiana na umuhimu wa mama mjamzito kuhudhuria kliniki kama inavyoainishwa katika Mwongozo wa Huduma za Kliniki kwa Wajawazito wa Mwaka 2018.

"Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, takwimu za MTUHA zinaonyesha kuwa, jumla ya wajawazito 2,028,151, sawa na asilimia 98 walihudhuria kliniki kwa mara ya kwanza, kulinganishwa na wajawazito 1,572,778 sawa na asilimia 86 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22," alisema.

Waziri Ummy alitaja mikoa iliyoongoza kwa kuwa na asilimia kubwa ya wajawazito waliohudhuria kliniki - hudhurio la kwanza ni Katavi (asilimia 105.9), Tabora (asilimia 88.3), Geita (asilimia 78.3), Shinyanga (asilimia 77.6) na Rukwa (asilimia 76.3).

Mikoa iliyokuwa na asilimia ndogo ya wajawazito waliohudhuria kliniki - hudhurio la kwanza ni Mtwara (asilimia 43.9); Njombe, (asilimia 44.6) na Kilimanjaro (asilimia 45.8).

# Waziri Ndalichako awapa angalizo wastaafu tarajali utapeli kimtandao

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amewataka wastaafu watarajiwa kuchukua tahadhari dhidi ya utapeli, ukiwamo wa kimtandao.

Alitoa angalizo hilo juzi alipofungua semina elekezi kwa wastaafu watarajiwa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) jijini Dar es Salaam.

Prof. Ndalichako, akizungumza na wastaafu hao kutoka Mkoa wa Dar es Salaam, aliipongeza PSSSF kwa kuandaa semina hiyo iliyobeba kaulimbiu ya 'Wekeza Mafao Yako Sehemu Salama kwa Uhakika wa Ukwasi'.

Alisema wastaafu wamekuwa walengwa wa matapeli, hivyo akawaasa kuwa makini na watu wanaofanya ushawishi wa kutengeneza mazingira ya kuwapo dharura.

"Mtu anapokutengenezea mazingira ya dharura, jitafakari kwanza kwanini iwe dharura. Serikali haiwezi kutaka kitu kwa dharura.

'Lipa sasa hivi'. Na unakuta mtu anatoa fedha na namba aliyopigiwa, akijaribu tena haipatikani na fedha zimekwenda," alihadharisha.

Waziri huyo alisema hiyo ndiyo sababu iliyoisukuma PSSSF kuandaa semina hiyo ili kuwajengea wastaafu wake watarajiwa uelewa na ufahamu kuhusu umuhimu wa kufanya uamuzi sahihi wa kukuza vipato vyao baada ya kustaafu ili kuleta tija na uendelevu wa kipato.

"Usia wangu kwenu ni kuyatumia vyema madini ya elimu mtakayoyapata hapa kwa kushikilia mambo makuu matatu: kuwa na mtazamo chanya, kuweka mipango makini na kutimiza ndoto binafsi baada ya kustaafu," alisema.

Prof. Ndalichako alisema kuwa kustaafu ni wajibu kwa kila mtumishi, hivyo hakuna budi kuendeleza maisha mazuri hata baada ya kustaafu.

Alisema ni vyema mtumishi akatambua kuwa safari ya kustaafu inaanza pale anapoanza ajira, hivyo ni muhimu kujiandaa kwa mipango na kifedha ili kufurahia maisha ya uhuru, lakini lazima kuwa na umakini katika usimamizi wa fedha.

"Matumizi ya busara ya fedha baada kustaafu ni muhimu zaidi kwa kuwa kwa kiasi kipato kinapungua na nguvu za kufanya kazi zinakwenda kupungua siku hadi siku," alihadharisha.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema mfuko huo unatarajia kuwa na wastaafu 11,000 kwa mwaka huu wa fedha 2023/24.

Alisema wastaafu watapatiwa mafunzo ya elimu ya uwekezaji katika masoko ya fedha, taarifa za nyaraka na utaratibu wa kufuata wakati wa kustaafu, kujiandaa kisakolojia baada ya kutoka katika utumishi, umuhimu wa kutunza mazingira wanayoishi kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uhalifu wa kimtandao ambao unawaathiri wastaafu wengi.

"Mfuko katika kutambua na kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, una mpango wa kutoa mche mmoja wa mti kwa kila mstaafu wa PSSSF.

"Mpaka sasa tuna wanachama 739,000 na lengo hapa ni kila mmoja apande na kutunza mche tutakaompatia pindi atakapofikia wakati wa kustaafu," alisema Kashimba.

Semina ya aina hiyo ilifanyika mwaka 2021 kwa wastaafu watarajiwa 3700 bara na visiwani na mwaka huu pia elimu itawafikia wastaafu kwenye mikoa ya Tanzania Bara na Visiwani, alisema CPA. Kashimba.



## Kamati ya Bunge yakoshwa utendaji kazi OSHA

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Daniel Sillo amesema Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) ni mdau mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi kwa sababu wanalinda nguvu kazi ya taifa kwa kuhakikisha maeneo ya kazi yanakuwa salama dhidi ya vihatarashi vya ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

Alitoa kauli hiyo jana wakati kamati hiyo ikihitimisha ziara ya kutembelea viwanda mkoani Arusha na Kilimanjaro kwa lengo la kuona utekelezaji wa sheria na miongozo mbalimbali ya usalama na afya mahali pa kazi katika viwanda.

Katika ziara hiyo waliongozana na Naibu Waziri - Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, Katibu Mkuu wa ziara hiyo, watumishi pamoja na wakaguzi wa OSHA.

Naibu Waziri, Patrobas Katambi alitoa rai kwa wamiliki wa maeneo ya kazi nchini kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa OSHA kwa sababu taasisi hiyo ipo kwa ajili ya kulinda usalama na afya za wafanyakazi pamoja na maeneo yao ya kazi.

Aidha, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda alisema OSHA imekuwa ikipokea shuhuda mbalimbali kutoka kwa wamiliki wa maeneo ya kazi wakikiri kuwa ukaguzi unaofanywa na OSHA vimesaidia katika kuongeza ushindani wa bidhaa wanazozalisha katika masoko ya kimataifa.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Kilimanjaro Plantation Limited, Calton Rabenold ambayo ni miongoni wa eneo la kazi lililotembelewa na kamati hiyo, aliishukuru serikali kupitia OSHA kwa kuendelea kuboresha mifumo ya usalama na afya katika maeneo ya kazi nchini.

alisema "OSHA imetusaidia sana kuboresha mifumo ya usalama na afya mahali pa kazi katika kampuni yetu kupitia kaguzi, mafunzo pamoja na ushauri wanaotoa baada ya kubaini upungufu na changamoto mbalimbali za kiusalama kupitia ukaguzi wanazozifanya na sisi tumekuwa tukifanya maboresho kila tunaposhauriwa " alisema Rabenold.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhandisi Cyprian Luhemeja aliishukuru kamati hiyo kwa kufanya ziara ya kutembelea viwanda hivyo pamoja na kushiriki semina elekezi ya mafunzo ya usalama na afya iliyofanyika Septemba 10 mwaka huu mkoani Arusha.

Hivyo, aliiomba kamati hiyo kuitikia wito pindi ofisi yake itakapo wahitaji tena.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ilitembelea kiwanda cha kuzalisha mbegu na mboga cha Rajik Zwaan kilichopo mkoani Arusha pamoja na kiwanda na mashamba ya Kilimanjaro Plantation Limited mkoani Kilimanjaro.

# Wizara ya Afya yaanza utekelezaji vipaumbele bajeti

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WIZARA ya Afya imeanza utekelezaji wa vipaumbele vyake 14 vya bajeti kwa kuwakutanisha madaktari bingwa, waganga wafawidhi wa hospitali za rufani za mikoa, makatibu wa hospitali na maofisa utumishi.

Lengo ni kuweka mipango na uelewa wa pamoja wa namna ya kuvitekeleza kwa tija vipaumbe hivyo katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Tiba, anayesimamia utoaji huduma katika hospitali za umma na za binafsi nchini, Dk. Caroline Damian, alisema wamelazimika kuandaa kikao kazi hicho maalum kwa ajili ya usimamizi wa hospitali za rufani za mikoa, kuvipitia vipaumbele hivyo na kuvitekeleza kwa ufanisi na tija kubwa.

Alisema wataalam hao pamoja na mambo mengine walipata fursa ya kuupitia mradi wa kuimarisha huduma za mama na watoto wachanga katika hospitali za rufani za mikoa.

Mradi huo wa miaka mitano (2022/2026) wa kuimarisha huduma za mama na watoto wachanga katika hospitali za rufani za mikoa, unatekelezwa na serikali kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Japan (JIKA).

"Tumeandaa kikao kazi hiki kwa ajili ya usimamizi wa hospitali za rufani za mikoa, kupitia vipaumbele vya sekta ya afya kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Wizara ina vipaumbele vingi lakini mahususi kwa mwaka huu wa fedha, tuna vipaumbele 14. Sasa katika utekelezaji wake kuna vile ambavyo utekelezaji wake unahusisha moja kwa moja hospitali zetu za rufani, ambazo zinatoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi.

...Kimuundo hizi hospitali za rufani za mikoa zinatakiwa kutoa huduma za kibingwa, kwa hiyo kipaumbele kimojawapo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi."

Kwa mujibu wa Dk. Caroline, kutokana na uwekezaji mkubwa wa miundombinu kwa maana ya watumishi wenye weledi, wao kama wataalam inabidi waonyeshe kwa vitendo Watanzania, uwekezaji uliofanyika unaendana na huduma wanazozipata katika hospitali hizo



Mkazi wa Kijiji cha Mamboleo, Kata ya Bwembwera wilayani Muheza mkoani Tanga, Josephine Raphael (wa tatu kushoto), akipokea funguo ya nyumba yake mpya kutoka kwa Afisa Tawala wa wilaya hiyo, Kasti Nelson juzi, ikiwa ni sehemu ya fidia kwa ajili ya kupisha ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), ambapo nyumba mbili zimekabidhiwa katika eneo hilo. Kushoto ni Mwakilishi kutoka Mradi wa EACOP, Deogratias Mruay na (kulia) ni Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Cyprian Mselem. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waliohama Ngorongoro waeleza utamu wa makazi mapya

**Na Allan Isack,** HANDENI

WANANCHI wanaoishi katika Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, ambao walihama kwa hiari kutoka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wameeleza siri ya namna wanavyoongeza kipato tofauti na walivyokuwa Ngorongoro.

Baadhi yao walisema katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja tangu kuondoka Ngorongoro, wamejikuta wakivutika kufanya shughuli zinazowasaidia kujikwamua kiuchumi.

Akieleza mafanikio hayo, mmoja wakazi hao, Victoria Huho alisema baada ya kufika Msomera walianza kufanya shughuli ndogo ndogo ikiwamo kulima mboga, ndizi, matunda na kulima mahindi.

"Japokuwa mvua zilikuwa chache mwaka huu, tumefanikiwa kuvuna gunia zaidi ya 60 za mahindi kwa awamu ya kwanza kwenye ekari saba tulizolima na kubadilisha maisha yetu ukilinganisha na tulivyokuwa Ngorongoro hatukuruhusiwa kufanya shughuli ya aina yoyote ya kutuongezea kipato.

"Hapa Msomera kuna uhuru wa kulima, kufanya biashara wakati wote na kufuga kwa kweli tunamshukuru Mungu kwa kuwa maisha yamebadilika yamekuwa mazuri na yanavutia kuishi kwa kuwa kuna huduma zote za kijamii," alisema.

Victoria alisema kwa sasa anafanya kilimo chenye tija cha kumwagilia na anapata mazao ikiwamo mboga, mahindi na matunda ambapo kiasi kidogo kinakuwa kwa matumizi ya familia na kingine anauza kama sehemu ya kuongeza kipato cha familia.


Aidha, Jackon Kipyo, alisema baada ya kufika kijijini hapo, alianzisha bustani ya mboga ambayo anayoitumia kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa shule yake,pia amelima mahindi ya chakula na mengine anauza.

"Huko Ngorongoro kweli nilikuwa mpambanaji lakini sikuwa na fursa inayoweka mazingira rafiki ya kufanya kazi kwa kuwa kila kitu tulichotaka kufanya ilitupasa kuomba kibali kutoka kwa uongozi wa mamlaka," alisema.

Vilevile, alisema akiwa Ngorongoro, hakuweza kuendeleza mradi wake wa shule ya msingi ila alipohamia huko Msomera amefanikiwa kukamilisha ujenzi wa shule yake.

"Huko Ngorongoro nilishindwa kumaliza ujenzi wa shule mpaka tupofikia hatua ya kuibomoa kwa kuwa utaratibu haukuwa unaruhusu kuendelea kufanya ujenzi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Msomera, Martin Ole Ikayo, alisema serikali imefanikiwa kuweka na kuboresha huduma muhimu za kijamii kwa watu waliotoka Ngorongoro na kuhamia kwenye kijiji hicho.





# Wafanyakazi kampuni uzalishaji mbegu wagoma kisa mshahara

**Na Nenesta Jasson,**
BUKOBA

WAFANYAKAZI wa Kampuni ya Grobal Agency Farm Limited iliyopo katika Kata ya Bugorora Wilaya ya Missenyi mkoani Kagera wamefanya mgomo wa kufanya kazi wakishinikiza kutolipwa malipo wanayodai kwa zaidi ya miezi sita.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe, wafanyakazi hao walieleza kuwa licha ya serikali kuingilia kati suala hilo lakini Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Fidelis Bashasha, aliendelea kukaidi maagizo kwa kukaa kimya bila kuwalipa stahiki zao.

Kampuni hiyo inayojihusisha na uzalishaji wa mbegu za mazao.

Mmoja wa wafanyakazi katika kampuni hiyo, Juma Milanga, alieleza jinsi wanavyofanya jitihada mbalimbali katika kudai mishahara yao ikiwa ni pamoja na kuwasilisha kero hiyo katika ofisi ya Katibu Kata pamoja na Mkuu wa Wilaya hiyo, lakini mwajiri wao ameendelea kuwazungusha.

"Kila tukimfuata mwajiri wetu amekuwa akituzungusha na wakati mwingine akitoa ahadi za kulipa stahiki zetu lakini hatekelezi jambo hilo hali inayosababisha kuendelea kupata matatizo kwa sababu tunashindwa kupata mahitaji yetu muhimu," alisema.

Mfanyakazi mwigine, Kajuna Maginga, alieleza kuwa licha ya kutoka mbali na kufanya kazi katika kiwanda hicho hajawahi kulipwa mshahara wowote.

Hivyo aliiomba serikali kuweka nguvu katika kuwasaidia kupata malipo yao kwani kazi zinaendelea kufanyika lakini malipo hawapati.

Kufuatia malalamiko hayo Nipashe ilijaribu kumtafuta Mkurugenzi wa kampuni ya hiyo, Fidelis Bashasha, juhudi ambazo ziligonga mwamba kwa kutokumpata ofisini kwake huku simu yake ikiita bila kujibiwa.

Nipashe lilimtafuta Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Wilson Sakulo, ambaye alisema ni kweli amepokea malalamiko kutoka kwa wafanyakazi hao.

Alisema baada ya kupokea malalamiko alifanya mawasiliano na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, ambapo alimpa muda wa kutosha kulipa madeni hayo.

Hata hiyo, aliwataka wafanyakazi hao kwenda Mahakamani ili waweze kupata haki yao.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (kushoto), akiwa na Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, wakishiriki ujenzi wa soko kuu la manispaa hiyo kwa kuweka kokoto kwenye ndoo, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Chuo cha nyuki chakanusha uvumi kuvuja mtihani

**Na Halima Ikunji,** TABORA

CHUO cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki mkoani Tabora kimekanusha taarifa juu ya kuvuja kwa mtihani wa mwisho wa ngazi ya stashahada, uliofanyika Agosti 14 hadi Agosti 18 chuoni hapo.

Mkuu wa chuo hicho, Semu Daudi, alitoa ufafanuzi huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kueleza kuwa taarifa hizo zipuuzwe na mtihani huo umefanyika chini ya usimamizi bila ya udanganyifu wa aina yoyote.

Alieleza kuwa uvumi huo umekuwa ukisambaa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa zikieleza kuwa baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho waliiba na kushiriki kuuvujisha.

"Taarifa hizi hazina ukweli ndani yake kwani mtihani ulifanyika ndani ya siku tano, hivyo dhamira yao ni kutaka kukichafua chuo na hawakitakii mema na uvumi huo ni baada ya kumaliza mitihani yao, hivyo puuzeni,"alieleza

Aidha, alisema kwamba walipopata taarifa hizo walijaribu kufuatilia mitihani iliyofanywa kwa kulinganisha karatasi zao na wanafunzi waliokuwa wanahisiwa kupewa mitihani hiyo lakini bado hawajapata uhakika, kwamba wanaendelea na uchunguzi zaidi.

"Bodi inaendelea na uchunguzi wake kwa siku nne kuanzia Septemba 11 hadi 14 na matokeo yoyote yatakayotolewa kwenye kamati ya bodi yataonyesha nini cha kufanya kama kutakuwa na walimu walivujisha mitihani au kuhisiwa hatua kali za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa kwa yoyote atakayebainika na bila ya kumuonea mtu aibu" alisema Daudi.

Nao baadhi ya wanafunzi wa mwaka wa tatu waliofanya mtihani huo akiwemo Hamisi Mndeme walisema hawakuona dalili zozote za uvujishaji wa mitihani hiyo, licha ya wao pia kusikia uvumi huo katika maeneo jirani.

# DC awashukia madiwani wanaokwamisha wananchi

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

MKUU wa Wilaya ya Geita, Cronel Magembe, ameagiza kukamatwa madiwani watakaokwamisha juhudi za wananchi katika kuchangia shughuli za maendeleo.

Alitoa agizo hilo juzi katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Nyankumbu Halmashauri ya Mji Geita, kufuatia baadhi ya wananchi wa Mtaa wa Elimu Kata ya Nyakumbu kumlalamikia Diwani wa Viti Maalumu CCM kuwazuia wananchi hao kuchangia fedha kwa ajili ya ununuzi wa eneo la ujenzi wa shule mpya ya msingi inayojengwa.

Wananchi hao wanachanga fedha ili kuondoa adha ya mlundikano wa wanafunzi katika shule ili kuwapunguzia kadhia ya kutembea umbali mrefu wanafunzi hao.

Alisema kuwa madiwani wa aina hiyo watakaobainika wanakwamisha juhudi za wananchi wakamatwe na kufikishwa ofisini kwake.

"Diwani huyo naye anatakiwa kuchangia mchango huo, akigoma akamatwe afikishwe ofisini kwangu aeleze kwanini anagoma na kwanini anawazuia wananchi kuchangia shughuli za maendeleo,"alisema Magembe .

Kadhalika, aliwataka wananchi kutobweteka kwa kusubiri kupata fedha kutoka Halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa eneo la ujenzi wa shule, kituo cha afya na zahanati.

Alisema serikali haiwezi kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa maeneo ya ujenzi wa huduma za kijamii, hivyo wananchi wanatakiwa kukubalina kiwango cha mchango na kuchangia wenyewe

"Napenda kuwaeleza ukweli, diwani wenu huenda alishindwa kuwaambia kuwa serikali haiwezi kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa maeneo ya ujenzi wa huduma za jamii bali inatoa fedha ya ujenzi wa mradi eneo likishapatikana," alisema Magembe.

Akizungumzia kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, alisema kuwa serikali katika Kata ya Nyankubu imetoa Sh. milioni 136 kwenye ujenzi madarasa, Shule ya Msingi Ukombozi na shule mpya ya Nyatotoro zilitolewa Sh. milioni 586.

Alisema pia serikali ilitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya kisasa katika Shule ya Msingi Uwanja.

Awali, mmoja wa wananchi katika mkutano huo, Kubengwa Mwita, aliibua hoja ya diwani huyo kuwazuia baadhi ya wananchi kutoa michango hiyo.

Alisema hadi sasa wananchi wameshachanga Sh. milioni 20 kwa ajili ya ununuzi wa eneo itakapojengwa shule mpya ya msingi.

Alisema: "Na kwa sasa tuna Sh.milioni 20 na eneo hilo linauzwa Sh.milioni 65, Diwani mmoja wa Viti Maalumu alikuja kuzuia mchango huo tunaomba utusaidie hali ambayo imesababisha uchangiaji kuendelea kusuasua," alisema Mwita.



Ukurasa 12

**Uwajibikaji mawakala ni muhimu uchaguzi wa Mbarali na kata sita**



Ukurasa 13

Kutoka msusi mtaani hadi diwani, njiani aking'oa vigogo wazoefu


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 13, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**G20 Delhi inavyoasisi kufungamana AU, India**

MKUTANO BARAZA LA VYAMA

# Dk. Samia alipogeuza kikao darasa la uongozi, maadili na demokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI hii imeanza na Mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa unaofunguliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Kila aina ya wasikilizaji walitega sikio lao kwa makini kufuatilia mkuu wa nchi atakachonena.

Hapo kukawepo wenyeji wanasiasa, wazee wa nchi kaka Joseph Warioba na Stephen Wasira, viongozi wa dini, hata wanahabari si haba, wakawapo katika kundi la wageni rasmi wanaokinga sikio kumsikiliza.

Ni aina ya hotuba ambayo hadhira na umma wa Kitanzania uliingia shauku nao, huku mrejesho wa alichowasilisha Rais Dk. Samia ikiwa katika sifa ya kuwa 'zaidi ya hotuba', ikibeba sura ya darasa na uana habari; hasa akifahamisha na kuelimsha zaidi.

Msingi wa shule hiyo kutoka kinywani kwa Rais juzi katika Kituo cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam, mada zake kwa sura moja ilishika falsafa na saikolojia, pia demokrasia zilizochukua vilevile tafsiri ya katiba na uongozi katika upande wa pili wa shilingi.

Ni maeneo ambayo Rais akayaona hayajakamilika katika siasa za nchi na yanapaswa kufanyiwa kazi akitenda kwa mfano lile pengo la elimu linalolalamikiwa; inatokana ama kwa kutojua au makusudi ya watendaji, hata yakabaki kuwa kasoro, hivyo umma unapaswa kubadilika.

Kurejea maana yake kitaaluma, uongozi unatajwa kuwa: "Mamlaka au karama ya kuwaonyesha watu njia kwa vitendo, kipimo chake kikitajwa ushawishi kwa watu na kufikia maendeleo yaliyotarajiwa."

Vilevile uongozi unabeba maana kuwa "dhana na taaluma anayopewa mhusika katika kusimamia na kufanikisha jambo




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipohutubia Mkutano Mkuu wa Vyama vya Siasa na Wadau wa Demokrasia nchini, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: MTANDAO**

kwa maslahi ya wote au mtu mmoja."

Katika demokrasia, nayo inashika maana kuwa "mfumo wa kiserikali unaowaweka na wananchi katika usawa mbele ya sheria na haki, wakishiriki kuamua masuala ya umma."

Hapo kunakuwapo mifumo yao ya kupitia wa kuwasilisha haki kama vile kwenye uchaguzi na uwakilishi katika kuamua, kama baraza la madiwani

Mtazamo wa jumla unasimama katika maana kwamba demokrasia ni utawala wa watu wakiwa na ridhaa yao; mwanazuoni mmoja akiupa tafsiri yake kutoka kwenye utafiti kwamba "utawala wa watu, kwa ajili ya watu na kwa manufaa ya watu."

Ni mara zote Rais Dk. Samia katika darasa lake amekuwa akitahadharisha matendo mabaya ya kiuongozi wa kisiasa, akitumia ushuhuda wake kwa yanayojiri, ikiwamo kwenye mitandao ya mawasiliano, pia mikutano ya hadhara aliyoiruhusu yanayotokea yako tofauti na kanuni walizopewa.

Hapo Rais akafafanua mzizi wa viongozi katika siasa na tofauti zao kwamba wapo anaowataja 'wamekulia katika vyama' huwa wanafundwa na wengine 'wamepitia kwenye vyama' huwa na sura ya ukiukaji maadili, huku akijumuisha umma unaokuwa katika msingi ya dini na maadili ya malezi, daima huzingatia kuvumilia misingi yao.

Katika darasa hilo la Dk. Samia anayekiri kuvumilia kauli zisizofaa kisiasa kupitia ustahimilivu wake kiuongozi, anasema hata dhana demokrasia japo ina misingi sawa ya asili, hutofuautiana kati ya jamii au sehemu moja na nyingine, kulingana na mustakabali wa jamii, mila, utamaduni na historia ya maisha yao

Kwa mujibu wa Rais Dk. Samia, si sahihi mtu kuropoka yasiyofaa kwa dai anatimiza haki yake kidemokrasia, ilihali ni kauli zenye sumu na kuvunja haki za binadamu katika jamii hiyo.

Kwa kurejea maandiko ya kitaaluma kuoanisha na neno la Dk. Samia, nadharia za wasomi wa sayansi ya siasa zinaonyesha kwamba makundi ya uongozi yanajigawa katika maeneo kadhaa.

Hapo kuna: Waonaojitwalia madaraka kama kinachotokea nchini Niger hivi sasa; uongozi kwa kurithi hasa katika utawala wa kifalme; wanaoteuliwa na mamlaka za juu zaidi; na ile inayotawala duniani zaidi, wanaopata uongozi kwa kuchaguliwa.

Katika majumuisho ya namna ya nadharia za namna hizo za uongozi, kuna makundi yanayotekeleza mamlaka zao kwa staili za; uongozi wa kidemokrasia na kimila unaotajwa ni wa amri bila ya kushirikisha watu kufanya uamuzi, zaidi ukilenga maslahi binafsi ya anayeongoza.

"Uongozi wa kidemokrasia ni ule wa kushirikisha watu katika kufanya uamuzi na kwa kawaida,viongozi wa aina hii hulenga kukidhi mahitaji ya walengwa," nadharia za wasomi zinaeleza, ikiangukia hoja inayopewa msisitizo na Rais Dk. Samia.

"Viongozi wanaochaguliwa mara nyingi huwa wanapewa muda wa kuongoza na wale viongozi wanaojiteua hujipatia wao wenyewe muda wa kuongoza au hata hapo watakapoamua kuachia madaraka," wanafafanua wasomi.

**SIFA ZA KIONGOZI**

Kwa mujibu wa nadharia za sayansi ya siasa zilizopo, sifa ya kiongozi anatakiwa kuwa na ufahamu sahihi wa himaya anayoiongoza; awe mwaminifu katika kikundi anachokiongoza, kama leo hii Watanzania wanavyojivunia nchini wasifu wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Lingine linatajwa ni kwa kiongozi kuwa na maadili mema hata kumfanya akubalike mbele ya jamii anayoiongoza na ndiko inakoangukia ujumbe wa juzi kutoka kwa Rais Dk. Samia.

Hapo ni alipokiambia kikao cha Baraza la Vyama vya Siasa na

**INAENDELEA UK. 13**

# Uwajibikaji mawakala ni muhimu uchaguzi wa Mbarali na kata sita



Kusanyiko la baadhi ya mawakala wa vyama mbalimbali vya siasa. **PICHA: NEC**

**Na Mroki Mroki**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetangaza uchaguzi mdogo wa ubunge jimbo la Mbarali mkoani Mbeya na kata sita za Tanzania Bara kufanyika Septemba 19 mwaka huu. Miongoni mwa wadau muhimu wa uchaguzi huu ni mawakala wa vyama vya siasa.

Hawa ni wawakilishi wanaoteuliwa na chama baada ya kupata ridhaa ya mgombea kwa ajili ya kusimamia maslahi ya chama na mgombea.

Kwa mujibu wa kifungu cha 57(1) na (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343, na kifungu cha 58(1) na (2), cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, sura ya 292, chama cha siasa kinaruhusiwa baada ya kupata ridhaa ya mgombea au wagombea kuteua na kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi orodha ya majina ya mawakala wa kupiga kura siku saba kabla ya siku ya uchaguzi.

Orodha hiyo itawasilisha pia majina ya mawakala mbadala ambao watatumika iwapo aliyepangwa atapata dharura.

Aidha, kwa mujibu wa kanuni ya 50(4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, na kanuni ya 43 (4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, mawakala wa kupiga kura wanatakiwa kula kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi siku saba kabla ya siku ya uchaguzi kwa kujaza fomu namba 6. Pia, hiki kitawahusu mawakala mbadala.

Kwa uchaguzi unaotarajiwa kufanyika jimboni Mbarali na kata sita mawakala wa vyama

> Wakala wa kuhesabu kura anawajibika kushiriki kuhesabu kura mahali pa kuhesabu kura na wakala wa kujumlisha kura anawajibika kushiriki kujumlisha kura.

na mbadala walitarajiwa kula kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi jana, na huenda tayari wamefanya hivyo kwa vile ndiyo ilikuwa siku ya kuapa.

Msimamizi wa Uchaguzi huvitaka vyama vya siasa kuwasilisha kwa maandishi majina ya mawakala wa kupiga kura, anuani na vituo walivyopangiwa kufanya kazi.

Kwa mujibu wa kanuni ya 50(6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 43(6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Vyama vya siasa huwasilisha barua za utambulisho wa kila wakala na kuainisha kituo alichopangiwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

Barua ya utambulisho wa kila wakala itakayowasilishwa na chama iainishe kituo alichopangiwa na iambatishwe na picha mbili zenye ukubwa sawa na picha iliyopo kwenye pasi ya kusafiria zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu.

Kifungu cha 57(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kinaeleza kuwa chama kitaruhusiwa kuteua wakala mbadala endapo aliyeteuliwa awali amefariki au ameshindwa kutekeleza majukumu ya uwakala. Sambamba na orodha ya mawakala wa vituo, vyama vitawasilisha majina mawili ya mawakala wa ziada kwa kata ambao watatumika kama wakala mbadala iwapo itahitajika.

Vilevile, endapo wakala hana picha anaweza kuwasilisha nakala mbili za mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo ambavyo Tume inavitambua kama kadi ya mpigakura, kitambulisho cha taifa, leseni ya udereva na pasi ya kusafiria.

Siku ya kugawa vifaa vya uchaguzi kwa watendaji wa vituo, Msimamizi wa Uchaguzi atawapatia watendaji hao orodha ya mawakala wa kupiga kura kwa kila kituo husika ambayo itapaswa kubandikwa nje ya vituo vya kupigia kura kabla ya kuanza kwa zoezi la kupiga kura.

Aidha, msimamizi wa kituo cha kupigia kura hataruhusiwa kuwaomba mawakala utambulisho mwingine wa ziada wanapofika katika vituo walivyopangiwa siku ya uchaguzi.

Kuna aina tatu za mawakala kwa mujibu wa majukumu wanayotekeleza, mosi wa kupiga kura; ambaye atashiriki katika zoezi zima la kupiga kura kituoni, ambaye mara baada ya zoezi hilo kukamilika atabadilika kuwa wakala wa kuhesabu kura.

Wakala wa kuhesabu kura anawajibika kushiriki kuhesabu kura mahali pa kuhesabu kura na wakala wa kujumlisha kura anawajibika kushiriki kujumlisha kura.

Katika kituo cha kupigia kura wakala wa chama cha siasa atamtambua mpiga kura anayetaka kupiga kura kama ndiye mwenye jina lililoandikwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Ikumbukwe kuwa, inashauriwa mawakala watoke katika maeneo ya karibu na vituo watakavyofanyia kazi hiyo ya uwakala.

Wakala anapokuwa kituoni anatakiwa kumwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea au wagombea na chama. Pia, anatakiwa kushirikiana na Msimamizi wa Kituo na Msimamizi Msaidizi wa Kituo katika kuhakikisha kwamba mwenendo wa kupiga kura kituoni unazingatia sheria na taratibu zilizowekwa na atatakiwa kujaza fomu namba 14 na 16 kituoni, ni kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi.

Aidha, wakala anatakiwa kukiwakilisha chama chake kuhesabu kura baada ya kukamilika kupigia kura kwani wakala wa kupiga kura ndiye atakuwa wakala wa kuhesabu pia.

Kila mpewa jukumu au kazi anapewa mipaka ya utekelezaji wa majukumu husika. Mawakala wa vyama vya siasa nao wana mipaka ya utekelezaji wa majukumu yao wawapo katika vituo vya kupigia kura au kuhesabia kura.

Mawakala wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kuorodhesha majina ya wapiga kura kituoni. Wapo mawakala huacha kufanya kazi zao za msingi vituoni na badala yake huorodhesha majina ya wapiga kura waliofika katika kituo, jambo ambalo ni kinyume na sheria.

Mbali na hiyo, mawakala wa vyama vya siasa hawaruhusiwi kutumia simu za mkononi ndani ya vituo vya kupigia kura, kuhesabu kura na kujumlisha kura.

Katika uchaguzi huu mdogo wagombea 13 kutoka vyama vya siasa 14 vyenye usajili kamili waliteuliwa kuwania kiti cha ubunge Mbarali ni Halima Magambo (AAFP), Osward Mndeva (DP), Zavely Seleka (UDP), Exavery Mwataga (CCK), Mary Daudi (UPDP) na Modestus Kilufi (ACT-Wazalendo).

Wengine ni Morris Nkongolo (TLP), Hashim Mdemu (ADC), Fatuma Ligania (NLD), Mwajuma Milambo (UMD), Bahati Ndingo (CCM), Husseni Lusewa (ADA-Tadea) Bariki Mwanyalu (Demokrasia Makini), hata hivyo mgombea wa NRA, Makuke Makuke hakurejesha fomu za uteuzi, hivyo, kukosa sifa za kuteuliwa.

Aidha, vyama vya siasa 17 vilijitokeza kuchukua fomu ya kuwania udiwani katika kata sita za Tanzania Bara, wagombea 45 waliteuliwa kuwania nafasi hizo.

Kata hizo ni Nala iliyopo Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Mfaranyaki Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Mwaniko Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Old Moshi Magharibi Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Marangu Kitowo Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Mtyangimbole Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.

Vyama vyote vinavyoshiriki uchaguzi huu mdogo wa Jimbo la Mbarali na kata sita za Tanzania Bara vinatarajiwa kuweka mawakala katika kila kituo. Ikumbukwe kuwa kukosekana kwa wakala kituoni hakubatilishi zoezi la kupiga kura.

Ni mategemeo ya NEC kuona mawakala waliopewa dhamana na wagombea na vyama kuwawakilisha katika vituo vya kupigia kura, kuhesabia na kujumlishia kura wakifanya kazi yao kwa weledi na kwa kufuata sheria.

Kukosekana kwa weledi miongoni mwa mawakala kunaweza kuchochea vurugu na kufanya uchaguzi usiwe wa huru na wa haki.

ZAWADI HAMDU VUAI

# Kutoka msusi mtaani hadi diwani, njiani aking'oa vigogo wazoefu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUTOKA msusi wa nywele hadi diwani haikuwa kazi rahisi katika safari yake ya kuwania uongozi wa kisiasa iliyopitia changamoto kadhaa ikiwamo hata kutikisa ndoa.

Huyu ni Zawadi Hamdu Vuai (55), Diwani wa wadi ya Kiyongoni Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja, ambaye ni mwanamama wa kwanza kushika jukumu hilo.

Ana familia na watoto wanne, alianza kugombea udiwani wa wadi tangu mwaka 2010 kupitia CCM na sasa ni kipindi chake cha tatu akiendelea kutumikia nafasi hiyo, anasema Zawadi.

Anasema wakati anaanza kazi yake ilikuwa ususi alioufanyia nyumbani kwake huko Makunduchi wala hakuwa na ndoto ya kuwa kiongozi.

"Nilikuwa msusi maarufu nawasuka wanawake wenzangu majirani kwa marafiki, sikuchagua mteja ilikua ni ajira yangu na ikiniingizia kipato ingawa ni kidogo lakini kikinisaidia kuendesha maisha yangu,"anasema Zawadi katika mahojiano na Nipashe hivi karibuni.

Diwani huyo anasimulia kuwa katika safari yake ya kuusaka uongozi, alipita katika mabonde na milima kwa sababu mume wake hakuunga mkono uamuzi wake wa kugombea nafasi ya kisiasa wakati huo ikiwa wadi ya Mzuri Makunduchi.

Anasema kitendo cha kuomba ridhaa kwa wananchi hakikuwa kigumu kwake kwa sababu wakati huo alikuwa mratibu wa wanawake na watoto wa kupinga vitendo vya udhalilishaji hivyo alikuwa na kundi kubwa la waliomuunga mkono.

"Kabla ya kugombea nafasi ya udiwani nilipata uteuzi wa kuwa mratibu wa wanawake na watoto shehia ya Mzuri Makunduchi na nafasi hiyo niliitumikia vyema,"anasema mwanamama huyo mcheshi anayefurahi muda wote.

Anasema kilichomshawishi kugombea nafasi ya uongozi ya udiwani ni baada ya kupokea malalamiko mengi ya unyanyasaji kwa wanawake na watoto kipindi hicho akiwa mratibu wa wanawake.

"Wakati huo changamoto za wanawake zilikuwa nyingi mno ikiwemo vipigo katika ndoa, nilikuwa msimamizi na mfuatiliaji na nilikuwa naumia sana kwa sababu mimi mwenyewe ni mhanga wa matukio hayo,"anasema.



Diwani wa wadi ya Kiyongoni Makunduchi Zawadi Hamdu Vuai. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

> "Niwasihi wanawake wenzangu baada ya kupata nafasi ya uongozi tusikimbie majukumu yetu ya ndoa, tusiwadharau waume na tulinde heshima ya ndoa zetu, tusiache kuwabembeleza waume zetu.

Aidha Zawadi, anasema baada ya kupokea changamoto hizo huwaongoza na kuwapeleka sehemu katika vyombo vya sheria na viongozi wa serikali ili kupata haki zao na wengi walifanikiwa.

Anasema kuwa kazi yake hiyo ya uratibu ilichangia kuunganisha ndoa ambazo zilikuwa hatarini kuvunjika kutokana na unyanyasaji ikiwemo vipigo dhidi ya wanawake. Harakati zake hizo, zilimwezesha kwenda Afrika Kusini kusomea uongozi akiwa ni kati ya wanawake watatu kutoka Tanzania walioshiriki mafunzo hayo yaliyokutanisha nchi saba, anaongeza.

Zawadi anasema atakuwa mchoyo wa fadhila bila ya kukishukuru Chama cha Waandishi Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, Zanzibar) ambacho kilimjengea uwezo wa kumpa mafunzo ya uongozi na kufanikiwa Kufika Afrika Kusini ambapo ni mara yake ya kwanza kusafiri nje ya Tanzania.

Diwani huyo anasema tokea udogo wake moyo wake ni wa kujituma na kuwatumikia wengine ili kupata haki zao.

### SAFARI KIUNGOZI

Zawadi anasema safari yake ya kuanza uongozi, ilikuwa na ugumu kwake kwa sababu wakati anaanza kugombea nafasi hizo zilikuwa zikishikiliwa na wanaume maarufu na vigogo wa chama.

"Kilikuwa kimbembe nilipoanza kugombea udiwani kwa sababu nafasi hizo zilikua zikishikiliwa na wanaume kwa miaka yote tangu ulipoanza mfumo wa vyama vingi lakini nilifanikiwa kuwaondoa kwa sababu nilishajengewa uwezo kutoka katika chama changu pamoja na TAMWA,"anasema.

Aidha, anasema moja ya masharti waliyopewa wakati aliposhiriki mafunzo ya uongozi nchini Afrika Kusini mwanzoni mwa mwaka 2010 ni lazima kugombea nafasi ya uongozi jimboni na kutakiwa kurejesha mrejesho wa mafanikio ya mafunzo hayo.

Anasema wakati anagombea udiwani wadi ya Mzuri, walikua wagombea watatu kupitia chama chake akiwa mwanamke pekee, lakini katika uchaguzi wa kura za maoni aliwagaragaza wanaume hao kwa kupata kura nyingi.

"Baada ya kupita katika kura ya maoni, wapiga kura katika wadi yangu walinikubali kipindi hicho wagombea kutoka vyama tofauti vya siasa tulikua sita mwanamke peke yangu lakini namshukuru Mungu nilishinda kupitia CCM,"anakumbusha.

Anasema siri ya mafanikio yake kuendelea kudumu kwa muda wa kipindi cha tatu cha uongozi, ni kuwa karibu na wananchi pamoja na jitihada zake katika kusimamia majukumu yake na chama kuendelea kumuamini.

Uchaguzi wa mwaka 2020 ushindani ulikuwa mkubwa zaidi kwa sababu katika chama chake walijitokeza wanaume tisa kugombea nafasi hiyo ya udiwani lakini katika kura ya maoni kwa mara nyingine alibuka mshindi na kuingia katika uchaguzi mkuu.

Anasema yote hayo aliyopitia kujiamini kunahitajika katika uongozi ili jamii nayo ijenge imani na kusema kuwa pia wanawake wanahitaji kujengewa ujasiri na kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi.

"Sioni fahari kila ninapogombea nafasi hii ya udiwani katika wadi najikuta mwanamke peke yangu, wanawake wenzangu tugombee nafasi za uongozi tusiogope ili kuwa na ushiriki sawa"alisema.

### MAISHA YA NDOA

Zawadi anasema mwanzo ilikuwa vigumu kumshawishi mume wake kumuunga mkono katika safari yake ya kugombea uongozi lakini alimshawishi hadi akamkubalia.

Anasema baada ya kumuelewesha na kumfahamu sasa ndoa yake imeimarika na yale manyanyaso aliyokua akiyapata katika ndoa kabla ya kuwa kiongozi yameondoka.

"Niwasihi wanawake wenzangu baada ya kupata nafasi ya uongozi tusikimbie majukumu yetu ya ndoa, tusiwadharau waume na tulinde heshima ya ndoa zetu, tusiache kuwabembeleza waume zetu,"anashauri,

Mwanasiasa huyu aliyesoma katika shule ya msingi na sekondari Makunduchi na kumali kidato cha nne 1983, amekuwa diwani wa wadi ya Mzuri Makunduchi kuanzia 2010 hadi.

Mwaka 2010 mpaka 2015 alikuwa diwani wa wadi ya Mzuri Makunduchi na kuanzia 2020 hadi sasa ameendelea na jukumu hilo kwenye wadi ya Kiyongoni Makunduchi, baada ya mabadiliko yaliyozipunguza kutoka mbili badala ya tatu za awali.

## Dk. Samia alipogeuza kikao darasa la uongozi, maadili na demokrasia

**INATOKA UK. 11**

Demokrasia Tanzania wiki hii, haja ya kurejea misingi ya imani kidini, hata utamaduni bora unaomlinda kiongozi asipotoke kuangukia mabaya.

Eneo lingine la sifa wanaziainisha wasomi, ambazo Dk. Samia naye akazigusa ni "amche Mungu; awe anakubalika na watu anaowaongoza; awe anaongoza watu katika misingi bora ya uongozi bila kujali jinsia, rangi, dini, wala kabila, awathamini watu wa makundi yote."

Mengine yanayoorodheshwa ni: "awe anakubali kushauriwa au kupokea ushauri kutoka kwa wengine; awe na uwezo wa kujifunza kutoka kwa wengine waliofanikiwa;awe na mawazo ya mbele ya kuona tatizo na kuonyesha baadhi ya njia za kulitatua, pamoja na kuona fursa."

### UHURU NA KATIBA

Rais Dk. Samia, anayetumia muda mrefu kukosoa kauli zinazokosa sifa za demokrasia na uongozi, anasema ameruhusu mikutano vyama vya siasa kwa lengo kuvipa wigo kukua kisiasa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani na uchaguzi mkuu mwaka 2025, lakini tayari anawashuhudia wanaoshindwa kuvitumia.

Anataja jamii ya leo ya Kitanzania, imerithi tija ya hulka bora ya umma na demokrasia waliorithi kwa watagulizi, lakini kuna wanaokusudia kuiharibu, huku akielekeza kidole wapo wanaokusudia kuteka dhana katiba mpya kuwa mali ya vyama vya siasa.

Hapo anasema, nadharia ya katiba haieleweki kwa kina mbele ya umma wote, licha ya kuwa mali ya kila Mtanzania, hivyo maboresho yake yanapaswa kuanza na elimu ya kina kabla ya kufikia maboresho yake, akisema ni mchakato ambao umeshaanza na maoni ya wanasiasa yanatakiwa kama sehemu muhimu, akisisitiza "katiba si mali ya vyama vya siasa, ni ya Watanzania wote...."

Ni kauli anayoitoa, huku hivi karibuni kukiwapo harakati za wanaolalamika kuchelewa kwa katiba mpya, wakitaka iwapo kabla ya uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025.



Mwenyekiti wa AU, Rais Azali Assoumani wa Comoro na Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi. **PICHA: AFP**

# G20 Delhi inavyoasisi kufungamana AU, India

## • China mshiriki mkuu anavyoelekea kutikiswa

**Na Mwandishi Wetu**

KWA kufanikisha kuusajili Umoja wa Afrika (AU) katika kundi la mataifa yenye nguvu kiuchumi duniani -G20, India imeshinda vita ya Afrika, imeteka mioyo ya bara ambalo muda wote linavutia mataifa yenye nguvu duniani.

Akimkaribisha Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Azaly Assoumani wa Comoro, kwenye meza ya wakuu G-20, Waziri Mkuu wa India Narendra Modi, anasema kujumuishwa kwa Umoja wa Afrika kwenye kundi hilo"kutaimarisha zaidi sauti ya Mataifa ya Kusini mwa Dunia.", kwa mujibu wa Eurasia Review.

Afrika kuingizwa kwenye G20 kwa msisitizo wa India ndani ya mkutano unaomalizika New Delhi hivi karibuni kunaipa India fursa kuchuana na China barani Afrika.

Kuiingiza Afrika kwenye G20 kukiratibiwa na India kutaipa nchi hiyo fursa za kujipenyeza zaidi barani Afrika kukabiliana na nguvu ya China ambayo pia imeimarika kikamilifu.

> Mwaka 2015 India iliandaa Kongamano la India na Afrika na imeendelea kupanua anga za kidiplomasia barani humo kwa kufungua balozi mpya katika nchi wanachama wa AU.

### USHIRIKIANO

Mwaka 2015 India iliandaa Kongamano la India na Afrika na imeendelea kupanua anga za kidiplomasia barani humo kwa kufungua balozi mpya katika nchi wanachama wa AU.

Mbali na kuunga mkono kujumuishwa kwa Umoja wa Afrika kama mwanachama wa kudumu wa G-20, India pia ilizialika Nigeria, Misri, na Mauritius kama sehemu ya 'washiriki au nchi wageni' katika mkutano wa G-20.

### ILIPOTOKA

Eurasia Review inataja Kongamano la India-Afrika lina mikutano mitatu ya kilele (2008, 2011 na 2015), wa kwanza ulifanyika Aprili 2008 huko New Delhi ambapo nchi 14 za Afrika zilishiriki. Katika mkutano huo, pande hizo mbili ziliazimia kudumisha mafungamano kwenye maeneo tisa ya ushirikiano.

Ni kuongeza biashara, India ilipanua mikopo mipya hadi kufikia dola za Marekani bilioni 5.4 na kuipa Afrika fursa ya unafuu kwenye makubaliano ya tozo za kodi kwa vile ina uchumi mdogo(LDCs tariff concessions.)

Mkutano wa pili wa kilele wa India na Afrika ulifanyika Addis Ababa Mei 2011. Katika mkutano huo, India iliahidi dola za Marekani milioni 700 na mkopo mpya wa dola bilioni 5 kusaidia uanzishwaji wa taasisi mpya na kuweka mipango ya elimu.

Aidha, India ilipa Afrika nafasi mpya 500 za mafunzo kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali chini ya mpango wake wa elimu ya kiufundi pamoja na ufadhili wa ziada kwa wanafunzi 400 kutoka mataifa mbalimbali.

Oktoba 2015 mkutano wa tatu wa kilele ulifanyika New Delhi,ukihudhuriwa na wakuu wa nchi na serikali kutoka zaidi ya mataifa 40 ya Afrika.

Aidha, ilipangwa kuwa mkutano wa nne ungefanyika mwaka jana Mauritania, lakini bado haujafanyika, hata hivyo India imeendelea kuishika Afrika mkono na katika mkutano wa kilele wa nchi za Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini (BRICS) huko Johannesburg mwezi uliopita India iliwasiliana na Afrika, shukrani kwa Rais wa Afrika Kusini Cyril Ramaphosa.

Katika muongo mmoja sasa, India imeongeza mikopo ya masharti nafuu ya zaidi ya dola za Marekani bilioni 12.3 kwa Afrika na kukamilisha miradi 197 na mingine 65 inaendelea kujengwa. Ikiwa ni pamoja na miundombinu, uunganishaji, ukuzaji ujuzi, afya, elimu, teknolojia ya habari, wafanyabiashara wadogo na wa kati na maendeleo vijijini.

### UWEKEZAJI

India ni miongoni mwa wawekezaji watano wakubwa barani Afrika wakiwa na uwekezaji wenye thamani ya takribani dola za Marekani bilioni 71 katika kipindi cha miaka 25 iliyopita.

Mauritius, Msumbiji, Sudan, Misri na Afrika Kusini zimekuwa wapokeaji wakuu wa uwekezaji wa India kuliko nchi nyingine.

Kampuni ya TATA ina viwanda vya magari Zambia na Uganda. Aidha, kampuni za dawa za India zimeongeza viwango vyao vya uzalishaji barani Afrika, kadhalika kwa upande wa dawa ina viwanda na inasambaza dawa za bei nafuu za kukabiliana na VVU/UKIMWI Afrika.

Kwa mfano, nchini Nigeria, asilimia ya wagonjwa wa UKIMWI wanaopokea matibabu imeongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na dawa hizi za bei nafuu kutoka India.

Aidha, ushirikiano mwingine ni katika mipango wa ujenzi wa makazi ya gharama nafuu nchini Zambia, Kenya, Togo na Mauritania.

Lakini pia India pia imetoa mkopo wa dola za Marekani milioni 300 kwa ajili ya kujenga reli inayoziunganisha Ethiopia na Djibout.

### USHINDA VS CHINA

Ripoti ya Africa's Dynamic Development , inayotolewa kwa pamoja na The Organization for Economic Cooperation and Development OECD na AU, inaonyesha kuwa kati ya 2017 na 2022, uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja wa China (FDI) Afrika ulifikia Yuan bilioni 74 (dola bilioni 10.14), ambayo ni sawa na asilimia 18 ya FDI ya kimataifa , ikiwa katika daraja moja na Ulaya na Marekani.

Kwa mujibu wa gazeti la China la Global Times, zaidi ya kampuni 3,000 za China zimewekeza kindakindaki Afrika, zaidi ya asilimia 70 ni za binafsi.

Aidha, zaidi ya asilimia 80 ya wafanyakazi wake ni wazawa wanaojenga madaraja na barabara, kuchimba visima na kuweka taa za barabarani.

Wakati huo huo, wameongeza uhamishaji wa teknolojia, mafunzo ya manunuzi ya ndani na wafanyakazi barani Afrika, na kusaidia kuboresha sekta za kilimo, viwanda na huduma, mbinu za kutengeneza na kusindika, kuongezeko thamani, na kuchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo na ustawi wa Afrika, inaongeza Global Times.

Mtandao wa conversation.com unaeleza kuwa ushirikiano wa China na Afrika ni zaidi ya kuchimba mafuta na madini, unahusisha uzalishaji viwandani, ajira, uwekezaji na mauzo ya nje, na fursa za kukuza kilimo na teknolojia kidijitali, maarufu. " Yunan Model".

Taarifa ya 'Policy Centre for the New South', inasema China ni mshirika mkubwa zaidi kibiashara wa Afrika, ikichangia zaidi ya dola za Marekani bilioni 282 mwaka 2022. Asilimia 16 ya bidhaa za viwandani za Afrika zilitoka China mwaka 2018, ikibadilisha mwelekeo wa awali uliegemea sana Ulaya.





## BAKWATA yawajia juu mashekhe, maimamu wazembe

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma limewataka viongozi wa ngazi ya kata na mitaa ya mashekhe, maimamu na walimu wa madrasa wanaofanya kazi kwa mazoea na kushindwa kwenda na kasi ya taasisi hiyo kujiondoa wenyewe badala ya kusubiri kufukuzwa.

Tahadhari hiyo imetolewa na Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Bashuru Hussen, wakati akizungumza na mashehe, maimamu na walimu wa madrassa kwenye kikao cha maandalizi ya Sikukuu ya Maulid itakayofanyika kitaifa mwezi huu mkoani Dodoma.

Bashiru, aliwataka viongozi hao ambao hawana uwezo na kasi ya utendaji wa baraza wakiwemo wale wanaofanya kazi kwa mazoea, kwamba hawatapewa muda wa kufanya nao kazi, hivyo ni vema wakajitafakari na kujitathimini wao wenyewe kama wanafaa kuendelea.

Aidha, aliwaonya viongozi wa ngazi za kata hadi mitaa kujiepusha na migogoro ndani ya misikiti yao, badala yake wawe chachu la kuhakikisha amani, umoja mshikamano na upendo unadumishwa kwa waumini kwenye maeneo yao.

Alisema: "Hapa ninaomba kupitia kikao hiki cha maandalizi ya Sikukuu ya Maulidi niwatake wale wote wanaochochea vurugu ndani ya misikiti na wale wanaojiona hawaendani na kasi ya baraza ni vema wawapishe wenye uwezo wa kukimbia sambasamba kama inavyotakiwa badala ya kusubiri kuondolewa kwa nguvu" alisisitiza.

Kadhalika, alisema BAKWATA linawataka waumini na viongozi wake kuacha kufanya kazi kwa mazoea, hivyo kwa kauli hiyo endapo itabainika kuna mashekhe, walimu na maimamu wazembe hawatafumbiwa macho bali watalazimika kujitafakari na hatimaye kujiondoa wenyewe bila kushurutishwa.

Hivyo, aliwataka mashekhe, maimamu na walimu kuhakikisha wanahubiri suala la amani ndani ya maeneo yao ya ibada, ili kuiunga mkono serikali ambayo imekuwa ikisisitiza kwa Watanzania kuombea taifa kwa muda wote.

# Warajisi watakiwa kutekeleza mfumo stakabadhi ghalani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MRAJISI wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Benson Ndiege, amewakata warajisi wasaidizi wa vyama vya ushirika kutekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani, ili kuwezesha ushirika kujiendesha kibiashara.

Alitoa maelekezo hayo juzi jijini hapa, wakati wa kikao kazi kati yake na warajisi wasaidizi, viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika vya upili kilicholenga kujadili muelekeo wa ushirika nchini.

"Maagizo haya ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wakati akishiriki mkutano wa kilimo Dar es Salaam ambapo alivitaka vyama vya ushirika nchini kuhakikisha kuwa wanatekeleza mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mazao mengine ya biashara kama wanavyofanya kwenye zao la korosho na ufuta" alisema.

Aidha, Dk. Ndiege alisema ni wakati sasa vyama vya ushirika vianze kuimarisha biashara ya mauzo ya mazao ya ushirika kwa kutumia mfumo wa stakabadhi ghalani.

"Kuna baadhi ya vyama katika Mkoa wa Songwe, Manyara na mikoa ya kusini wamefanya vizuri kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, kupitia mfumo huu bei ya ufuta imepanda kutoka Sh. 1,300 mwaka jana hadi kufikia Sh. 4,000 mwaka huu, tukitumia mfumo huu ushirika utajiendesha kibiashara na kuwa wenye tija kwa wakulima" alisema

Kadhalika, alisema ili ushirika uwe na mwelekeo chanya ni lazima jitihada zifanyike ili kuhakikisha kunakuwa na uwekezaji katika mifumo ya kisasa, kidijitali kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika vyama pamoja na mamlaka za usimamizi.

"Mpaka sasa tumesajili vyama 5,642 na wanachama 704,648 katika mfumo wetu wa MUVU ni lazima tuhakikishe vyama vyote 7,000 na wanachama tulionao zaidi ya milioni nane wanasajiliwa katika mfumo huu ili shughuli zetu zote zifanyike katika mfumo wa kidijitali, lakini pia tuhakikishe mfumo huu unakwenda sambamba na mizani ya kidijitali ili tuweze kwenda kisasa" alisema Dk.Ndiege.

Hata hivyo aliwataka warajisi wasaidizi kuhakikisha mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika inayotarajiwa kuanzishwa rasmi ifikapo mwishoni mwa mwaka huu unakamilika.

"Tunahitaji Sh. bilioni 15 ili kuweza kuanzisha benki hii, mpaka sasa tuna Sh.bilioni 6.7 tukiwa na upungufu wa Sh.bilioni 8.3, ofisi yangu ilitoa waraka kwa ajili ya wanachama kuchangia ama kununua hisa ili waweze kumiliki hisa kwa pamoja na namna tunavyoweza kuwahamasisha ili wawe miongoni mwa wamiliki lakini pia tuweze kukamilisha kiwango kilichobaki ili benki yetu iweze kuanzishwa" alisema

Dk. Ndiege alisema ili kuhakikisha ukuaji na maendeleo ya ushirika ni lazima kuwepo usimamizi na udhibiti wa vyama hivi pamoja na kuhamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika.

"Tunaweza kuhamasisha ushirika katika miradi ya BBT, eneo la mboga, mifugo na uvuvi pamoja na kuwahamasisha uanzishwaji wa SACCOS ndani ya AMCOS, kutoa elimu kupitia majukwaa ya ushirika ya mikoa pamoja na kuongeza uelewa wa umma kuhusu shirika kupitia vyombo vya habari" alisema Dk. Ndiege

Vilevile, alisema ili kuimarisha shughuli za vyama vya ushirika pamoja na usimamizi kila mdau anajukumu la kuhakikisha kuwa ushirika unajibu mahitaji ya jamii kwa uimara wake na uendelevu kwa kutatua kero za kiuchumi na kijamii.



Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo (kushoto), akifurahia jambo na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Misigiri, wilayani Iramba mkoani Singida juzi. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Profesa Kitila, Mwigulu wamaliza tofauti zao

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo ameweka bayana kumaliza tofauti za kisiasa kati yake na Waziri wa Fedha, Dk.Mwigulu Nchemba, zilizojitokeza wakati wa uchaguzi mkuu.

Prof. Mkumbo ambaye ni Mbunge wa Ubungo jijini Dar es Salaam na Dk. Mwigulu ambao wote ni wazaliwa wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida walivutana kugombea ubunge katika jimbo la Iramba Magharibi mwaka 2015.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na wananchi wa Misigiri wilayani Iramba wakati hafla ya kumkabidhi mkandarasi ujenzi wa Barabara ya Singida hadi Kiziga, alisema tangu mwaka 2013 hadi mwaka 2020 yeye na mdogo wake (Dk.Mwigulu Nchemba) walipambana kisiasa lakini wanamshukru Mungu wote wamekuwa wabunge na mawaziri.

"Tangazo ambalo nawaletea ni kwamba mimi na mwigulu mdogo wangu tulishayamaliza, hatununiani, hatukasirikiani, tunacheka, tunakula pamoja na tunakula nyama pamoja,kwa hiyo hilo limeisha fanyeni kazi za maendeleo ungeni mkono Mwigulu,ungeni mkono CCM fanyeni kazi kwa maendeleo ya Iramba," alisema.

Prof. Mkumbo aliongeza kuwa: "Mimi ni mbunge wa jimbo la Ubungo Dar es Salaam, kule kwetu ukija wale wazaramo watakuimbia nyimbo wakisema muacheni Kitila abaki alipo na mimi nawaambia leo mwacheni Mwigulu abaki pale alipo," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba, alisema mkoa umejipanga kulima ekari milioni moja za alizeti katika msimu wa kilimo wa mwaka huu kutoka ekari 681,000 zilizolimwa msimu uliopita, ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula ambayo yatatosheleza kulisha nchi nzima.

Alisema lengo ni kuhakikisha tatizo la mafuta ya kula nchini linamalizika na kwamba hilo linawezekana kwasababu wakulima wanajituma sana katika kilimo.

Akizungumzia kuhusu mbolea alisema maelekezo ya Wizara ya Kilimo yalishatolewa, kwamba ifikapo Septemba 20, mwaka huu mbolea itakuwa imefika kila wilaya.

"Mwaka huu niwahakikishie Wanasingida hakuna kijiji ambacho mbolea haitafika, kazi imeanza na maofisa kilimo safari hii sitawaachia tutasimamia mimi na ma-DC (Wakuu wa Wilaya) wangu kuhakikisha mbolea na mbegu inafika kwa wakati ili watu wasipate sababu, nataka safari hii tuongeze uzalishaji wa mazao," alisema.

Alisema hivi sasa kuna miradi 12 ya mabonde ya umwagiliaji kwa Mkoa wa Singida ambayo ujenzi wake upo katika hatua mbalimbali ambayo ikikamilika mazao kama vitunguu ufuta, dengu, pamba, korosho, mahindi na alizeti yatakuwa yanapatikana kutoka Singida.

Serukamba akizungumzia sekta ya maji, alisema katika vijiji 441 vilivyopo katika mkoa huu asilimja 66 vinapata huduma ya maji na mjini upatikanaji wa maji ni asilimia 85 na malengo ifikapo mwaka 2025 upatikanaji wa maji vijijini itafikia asilimia 80 na mjini asilimia 100.

Kuhusu umeme alisema vijiji 341 kati ya 441 vilivyopo mkoani hapa vimepata umeme na vijiji 100 vilivyobaki makandarasi wapo kazi wakiendelea na kazi na ni matumaini ifikapo mwakani vijiji vyote vitakuwa vimefikiwa na umeme.





# Wakulima, maofisa ugani wapigwa msasa kuhusu mikopo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB), imeanza kuwanoa wakulima na maofisa ushirika wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu mikopo ya kuendeleza kilimo.

Lengo ni kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha chakula barani Afrika.

Mafunzo hayo yameanza kutolewa mkoani Mbeya ikiwa ni wiki moja baada ya kumalizika kwa mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) lililofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wakuu wa mataifa mbalimbali.

Juzi mafunzo hayo yalianza kutolewa kwa maofisa ushirika wa wilaya zote saba za Mkoa wa Mbeya pamoja na warajisi wa vyama vya ushirika wa mkoa huo kabla ya kwenda kwa wakulima na kwenye mikoa mingine ya ukanda huo.

Ofisa Maendeleo ya Biashara Kitengo cha Wakulima Wadogo (TADB), Angelina Nyansambo, alisema mpaka sasa zaidi ya wakulima 2,000 wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wameshajengewa uwezo kwenye masuala mbalimbali ya kuendeleza kilimo.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya waliamua kuanza na maofisa ushirika kwa sababu wao ndio wapo karibu zaidi na wakulima na hivyo watawatumia kama mabalozi wa kueneza elimu hiyo kwa wakulima kwenye maeneo yao.

"Tumeanza utekelezaji wa mambo yaliyojadiliwa kwenye mkutano wa AGRF ambalo nchi yetu ilikuwa mwenyeji, sisi TADB tayari tumeshawajengea uwezo wakulima zaidi ya 2,000 kwa lengo la kuongeza tija kwenye uzalishaji," alisema Angelina.

Nyansabo alisema kuwa mpaka sasa tayari benki hiyo imeshatoa mikopo kwa wakulima zaidi ya milioni moja nchini kwa ajili ya kuwasaidia kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao hasa kilimo na ufugaji ambazo ndio sekta zinazolengwa.

Hata hivyo alisema mafunzo hayo yanaendelea nchi nzima ambapo benki inakusudia kuwafikia zaidi ya wakulima 28,000 nchi nzima na kuwapatia elimu kuhusu mikopo inayopatikana pamoja na namna ya kuongeza tija kwenye kilimo.

Baadhi ya maofisa ushirika wa wilaya za Mkoa wa Mbeya walioshiriki mafunzo hayo walisema elimu hiyo itakuwa na faida kubwa kwao na kwa wakulima wakidai kuwa bado wakulima wanahangaika namna ya kupata mitaji ya kuendeleza shughuli zao.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa wa Mbeya, Irene Luoga, aliiomba Benki ya TADB kuitumia mikutano mikuu ya vyama vya ushirika ili kutoa elimu kwa wakulima kwa maelezo kuwa wakitumia mbinu hiyo wanaweza wakawafikia wakulima wengi zaidi.

Alisema vyama vya ushirika ndio vyenye wakulima na kwamba hata wao baada ya kupata elimu hiyo wanakusudia kuitumia mikutano ya vyama hivyo kufikisha elimu hiyo kwa wakulima.

"Idadi kubwa ya wakulima hasa wa mazao ya kibiashara kwa sasa wamejiunga na vyama vya ushirika hivyo kama TADB wanahitaji kuwafikia wakulima hao nashauri washiriki kwenye mikutano mikuu ya vyama vya ushirika na kuitumia kufikisha elimu kwa wakulima," alisema Irene.

Ofisa Ushirika Wilaya ya Chunya, Kongwa Nkinda alisema wakulima wengi hasa wadogo hawana elimu kuhusu mikopo inayotolewa kwenye kilimo, hivyo akataka jitihada zaidi zifanyike kuwafikia na kuwaelimisha.

Alisema ikiwa wakulima wataelewa fursa zinazopatikana katika kuwawezesha kuongeza uzalishaji, watazitumia kuhakikisha wanapata tija katika kilimo, jambo ambalo litasaidia taifa kuzalisha kwa wingi mazao na kufikia lengo la kuwa kitovu cha chakula barani Afrika.

Naye Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, Geofrey Mwaijende, alisema tayari halmashauri yake imeshaanza kunufaika na fedha za mikopo zinazotolewa na TADB, kwamba chama cha ushirika cha wafugaji ndani ya halmashauri hiyo kimeshakopeshwa zaidi ya shilingi milioni 300.

Hata hivyo akaiomba Benki ya TADB kutoa hamasa pia kwa wafugaji kama sekta inayohusiana na kilimo ili kuongeza chachu ya wao pia kunufaika na fursa zinazotolewa na benki hiyo.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ndiyo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini hali iliyoifanya kubatizwa jina la ghala la taifa la chakula.

## Mbaroni tuhuma kumuua baba yake akimpiga na ubao kichwani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia mkazi wa Ilemi jijini Mbeya, Humphrey Kihali (25) kwa tuhuma za kumuua baba yake mzazi, Francis Kihali (50) kwa kumtwanga na ubao kichwani.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Anthony Mkwawa, alisema tukio hilo lilitokea Septemba 10 mwaka huu saa 10:45 jioni ambapo mtuhumiwa alimvizia baba yake akiwa chumbani na kumpiga kichwani.

Alisema marehemu alikimbizwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa ajili ya matibabu lakini alifariki Septemba 11 mwaka huu saa 1:30 asubuhi wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

Kamanda Mkwawa alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa mtuhumiwa ana matatizo ya akili lakini wanaendea na uchunguzi ili kubaini vitu vingine.

"Pamoja na kwamba uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mtuhumiwa ana matatizo ya akili lakini tunaendelea na uchunguzi zaidi ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe dhidi yake," alisema Kamanda Mkwawa.

Alisema uchunguzi utakapokamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria na kwamba kwa sasa anaendelea kushikiliwa.

Aliwataka wazazi wenye watoto wenye matatizo ya akili kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara kama yaliyotokea ya mauaji na kwamba kuna matatizo mengine wanaweza wakasababisha.

Vilevile aliwataka wazazi wenye watoto wa aina hiyo wanaotumia dawa kuhakikisha wanawasimamia kutumia dawa hizo ili kuepuka madhara zaidi kutokea.



Baadhi ya wafanyakazi wa KFC Tanzania inayomilikiwa na Kampuni ya Dough Works Ltd, wakikata keki kusherehekea maadhimisho ya miaka 10 ya utoaji huduma nchini, wakati wa uzinduzi wa mgahawa wake wa Mbezi Beach, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara Njombe kicheko serikali ikitatua kero zao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza kero za wafanyabiashara nchini tofauti na kipindi kilichopita hasa kwa kuondoa baadhi ya vikwazo.

Hayo yalisemwa kwenye mkutano wa wafanyabiashara Halmashauri ya Mji Njombe na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Hamis Livembe.

Livembe alisema hali ya wafanyabiashara kwa sasa inaridhisha tofauti na walikotoka.

"Lakini tunaangalia mood (hali) ya wafanyabiashara kule tulipotoka na sasa angalau wanatabasamu jambo wanawasilisha hoja zao lakini vichwa vimetulia, ingawa changamoto zote hazijamalizika kufanyiwa kazi na kuna nyingine ndogondogo mpya zinajitokeza lakini tunakoelekea ni kuzuri," alisema Livembe.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa wafanyabiashara wanatakiwa kutambua haki bila wajibu ni fujo.

"Kuna haki tunadai, serikali imeanza kutekeleza lakini na sisi tunatakiwa tutimize wajibu, katika sera zetu tunahimiza na hilo kwamba tusirudi kule tulikotoka ili tuendeelee kuelewana na kulipa kodi kwa hiyari na kutozwa kodi zinazolipika lazima na sisi tutimize wajibu wetu,"alisema Livembe. Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe, Specioza Owure, alitolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali za wafanyabiashara hao, huku akitoa onyo kali kwa wanaofanyakazi ya kuuza risiti mitaani.

"Sasa hivi Njombe kuna tatizo kubwa la kununua risiti hasa kwa wafanyabishara wa mbao, hicho ni kitu ambacho sasa kiko 'open' (wazi) sio siri mpaka kiwango mnacholipa kinajulikana kwamba risiti moja ni shilingi 300,000," alisema Owure na kuongeza.

"Unampelekea mtu ambaye anajinufaisha yeye na familia yake unawasahau Watanzania milioni 60 ambao wanahitaji hiyo 300,000 unayompa mtu mmoja, wengine mnatumika kwa sababu hawa wanaowauzia risiti akishaona mauzo yake yameonekana yapo juu hatumuoni kwa hiyo, naomba mchezo huo ambao umekithiri Njombe tuuache," aliongeza.

Awali baadhi ya wafanyabiashara mkoani Njombe akiwamo, Erick Mtega walisema hali ya biashara ni mbaya mjini Njombe huku wengine wakilalamikia changamoto za mashine ya EFD.

"Mashine ikiharibika unatakiwa ukanunue nyingine kwa gharama nyingine na siyo kwa makato kama mashine za kipindi cha kwanza, unanunua mashine ya pili unakatwa na TRA kwenye kodi kiasi fulani lakini hicho kitu inaonekana hakipo," alisema Mtega.





# Wakulima, maofisa ugani wapigwa msasa kuhusu mikopo ya kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB), imeanza kuwanoa wakulima na maofisa ushirika wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu mikopo ya kuendeleza kilimo.

Lengo ni kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha chakula barani Afrika.

Mafunzo hayo yameanza kutolewa mkoani Mbeya ikiwa ni wiki moja baada ya kumalizika kwa mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) lililofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wakuu wa mataifa mbalimbali.

Juzi mafunzo hayo yalianza kutolewa kwa maofisa ushirika wa wilaya zote saba za Mkoa wa Mbeya pamoja na warajisi wa vyama vya ushirika wa mkoa huo kabla ya kwenda kwa wakulima na kwenye mikoa mingine ya ukanda huo.

Ofisa Maendeleo ya Biashara Kitengo cha Wakulima Wadogo (TADB), Angelina Nyansambo, alisema mpaka sasa zaidi ya wakulima 2,000 wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wameshajengewa uwezo kwenye masuala mbalimbali ya kuendeleza kilimo.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya waliamua kuanza na maofisa ushirika kwa sababu wao ndio wapo karibu zaidi na wakulima na hivyo watawatumia kama mabalozi wa kueneza elimu hiyo kwa wakulima kwenye maeneo yao.

"Tumeanza utekelezaji wa mambo yaliyojadiliwa kwenye mkutano wa AGRF ambalo nchi yetu ilikuwa mwenyeji, sisi TADB tayari tumeshawajengea uwezo wakulima zaidi ya 2,000 kwa lengo la kuongeza tija kwenye uzalishaji," alisema Angelina.

Nyansabo alisema kuwa mpaka sasa tayari benki hiyo imeshatoa mikopo kwa wakulima zaidi ya milioni moja nchini kwa ajili ya kuwasaidia kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao hasa kilimo na ufugaji ambazo ndio sekta zinazolengwa.

Hata hivyo alisema mafunzo hayo yanaendelea nchi nzima ambapo benki inakusudia kuwafikia zaidi ya wakulima 28,000 nchi nzima na kuwapatia elimu kuhusu mikopo inayopatikana pamoja na namna ya kuongeza tija kwenye kilimo.

Baadhi ya maofisa ushirika wa wilaya za Mkoa wa Mbeya walioshiriki mafunzo hayo walisema elimu hiyo itakuwa na faida kubwa kwao na kwa wakulima wakidai kuwa bado wakulima wanahangaika namna ya kupata mitaji ya kuendeleza shughuli zao.

Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa wa Mbeya, Irene Luoga, aliiomba Benki ya TADB kuitumia mikutano mikuu ya vyama vya ushirika ili kutoa elimu kwa wakulima kwa maelezo kuwa wakitumia mbinu hiyo wanaweza wakawafikia wakulima wengi zaidi.

Alisema vyama vya ushirika ndio vyenye wakulima na kwamba hata wao baada ya kupata elimu hiyo wanakusudia kuitumia mikutano ya vyama hivyo kufikisha elimu hiyo kwa wakulima.

"Idadi kubwa ya wakulima hasa wa mazao ya kibiashara kwa sasa wamejiunga na vyama vya ushirika hivyo kama TADB wanahitaji kuwafikia wakulima hao nashauri washiriki kwenye mikutano mikuu ya vyama vya ushirika na kuitumia kufikisha elimu kwa wakulima," alisema Irene.

Ofisa Ushirika Wilaya ya Chunya, Kongwa Nkinda alisema wakulima wengi hasa wadogo hawana elimu kuhusu mikopo inayotolewa kwenye kilimo, hivyo akataka jitihada zaidi zifanyike kuwafikia na kuwaelimisha.

Alisema ikiwa wakulima wataelewa fursa zinazopatikana katika kuwawezesha kuongeza uzalishaji, watazitumia kuhakikisha wanapata tija katika kilimo, jambo ambalo litasaidia taifa kuzalisha kwa wingi mazao na kufikia lengo la kuwa kitovu cha chakula barani Afrika.

Naye Ofisa Ushirika wa Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, Geofrey Mwaijende, alisema tayari halmashauri yake imeshaanza kunufaika na fedha za mikopo zinazotolewa na TADB, kwamba chama cha ushirika cha wafugaji ndani ya halmashauri hiyo kimeshakopeshwa zaidi ya shilingi milioni 300.

Hata hivyo akaiomba Benki ya TADB kutoa hamasa pia kwa wafugaji kama sekta inayohusiana na kilimo ili kuongeza chachu ya wao pia kunufaika na fursa zinazotolewa na benki hiyo.

Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ndiyo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini hali iliyoifanya kubatizwa jina la ghala la taifa la chakula.

## Mbaroni tuhuma kumuua baba yake akimpiga na ubao kichwani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia mkazi wa Ilemi jijini Mbeya, Humphrey Kihali (25) kwa tuhuma za kumuua baba yake mzazi, Francis Kihali (50) kwa kumtwanga na ubao kichwani.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Anthony Mkwawa, alisema tukio hilo lilitokea Septemba 10 mwaka huu saa 10:45 jioni ambapo mtuhumiwa alimvizia baba yake akiwa chumbani na kumpiga kichwani.

Alisema marehemu alikimbizwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa ajili ya matibabu lakini alifariki Septemba 11 mwaka huu saa 1:30 asubuhi wakati akiendelea kupatiwa matibabu.

Kamanda Mkwawa alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa mtuhumiwa ana matatizo ya akili lakini wanaendea na uchunguzi ili kubaini vitu vingine.

"Pamoja na kwamba uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mtuhumiwa ana matatizo ya akili lakini tunaendelea na uchunguzi zaidi ili hatua zaidi za kisheria zichukuliwe dhidi yake," alisema Kamanda Mkwawa.

Alisema uchunguzi utakapokamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria na kwamba kwa sasa anaendelea kushikiliwa.

Aliwataka wazazi wenye watoto wenye matatizo ya akili kuchukua tahadhari ili kuepuka madhara kama yaliyotokea ya mauaji na kwamba kuna matatizo mengine wanaweza wakasababisha.

Vilevile aliwataka wazazi wenye watoto wa aina hiyo wanaotumia dawa kuhakikisha wanawasimamia kutumia dawa hizo ili kuepuka madhara zaidi kutokea.



Baadhi ya wafanyakazi wa KFC Tanzania inayomilikiwa na Kampuni ya Dough Works Ltd, wakikata keki kusherehekea maadhimisho ya miaka 10 ya utoaji huduma nchini, wakati wa uzinduzi wa mgahawa wake wa Mbezi Beach, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W'biashara Njombe kicheko serikali ikitatua kero zao

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

IMEELEZWA kuwa serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza kero za wafanyabiashara nchini tofauti na kipindi kilichopita hasa kwa kuondoa baadhi ya vikwazo.

Hayo yalisemwa kwenye mkutano wa wafanyabiashara Halmashauri ya Mji Njombe na aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania, Hamis Livembe.

Livembe alisema hali ya wafanyabiashara kwa sasa inaridhisha tofauti na walikotoka.

"Lakini tunaangalia mood (hali) ya wafanyabiashara kule tulipotoka na sasa angalau wanatabasamu jambo wanawasilisha hoja zao lakini vichwa vimetulia, ingawa changamoto zote hazijamalizika kufanyiwa kazi na kuna nyingine ndogondogo mpya zinajitokeza lakini tunakoelekea ni kuzuri," alisema Livembe.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa wafanyabiashara wanatakiwa kutambua haki bila wajibu ni fujo.

"Kuna haki tunadai, serikali imeanza kutekeleza lakini na sisi tunatakiwa tutimize wajibu, katika sera zetu tunahimiza na hilo kwamba tusirudi kule tulikotoka ili tuendeelee kuelewana na kulipa kodi kwa hiyari na kutozwa kodi zinazolipika lazima na sisi tutimize wajibu wetu,"alisema Livembe. Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe, Specioza Owure, alitolea ufafanuzi wa hoja mbalimbali za wafanyabiashara hao, huku akitoa onyo kali kwa wanaofanyakazi ya kuuza risiti mitaani.

"Sasa hivi Njombe kuna tatizo kubwa la kununua risiti hasa kwa wafanyabishara wa mbao, hicho ni kitu ambacho sasa kiko 'open' (wazi) sio siri mpaka kiwango mnacholipa kinajulikana kwamba risiti moja ni shilingi 300,000," alisema Owure na kuongeza.

"Unampelekea mtu ambaye anajinufaisha yeye na familia yake unawasahau Watanzania milioni 60 ambao wanahitaji hiyo 300,000 unayompa mtu mmoja, wengine mnatumika kwa sababu hawa wanaowauzia risiti akishaona mauzo yake yameonekana yapo juu hatumuoni kwa hiyo, naomba mchezo huo ambao umekithiri Njombe tuuache," aliongeza.

Awali baadhi ya wafanyabiashara mkoani Njombe akiwamo, Erick Mtega walisema hali ya biashara ni mbaya mjini Njombe huku wengine wakilalamikia changamoto za mashine ya EFD.

"Mashine ikiharibika unatakiwa ukanunue nyingine kwa gharama nyingine na siyo kwa makato kama mashine za kipindi cha kwanza, unanunua mashine ya pili unakatwa na TRA kwenye kodi kiasi fulani lakini hicho kitu inaonekana hakipo," alisema Mtega.



# BoT yatoa leseni ya huduma za kifedha kampuni ya India

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KATIKA kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za uhakika za malipo ya fedha kwa njia ya kidijitali, Kampuni ya Airpay Tanzania imepewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutoa huduma nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari Zanzibar, Mwanzilishi wa kampuni hiyo, Kunal Jhunjhunwala, alisema wanafuraha kupokea leseni hiyo ya huduma za malipo kutoka BoT, akisema inaashiria kujitolea kwao katika kupanua huduma za kifedha kidijitali Afrika.

Alisema mafanikio hayo yanaashiria hatua kubwa kwao ambayo ilianza Februari 2023 na tangu wakati huo wamefanya mikutano ya mashauriano na wadau mbalimbali kutoka Zanzibar na Bara.

Aidha, alisema Tanzania ina vivutio vya asili, hivyo ni fursa kwa Airpay kuchukua sehemu muhimu katika safari ya kidijitali nchini ya kujenga jamii na uchumi usiotegemea mzunguko wa pesa taslimu.

Mwanzilishi mwenza wa kampuni hiyo, Yasmin Chali, alisema kampuni hiyo bado imejitolea kutoa suluhu za malipo za kiubunifu, salama na zinazoweza kufikiwa kwa biashara na watumiaji Afrika huku zikiunganisha huduma za kifedha ndani na nje ya bara hilo.

Alisema leseni hiyo ya huduma za malipo iliyotolewa na BoT inasisitiza kujitolea kwao kufuata mahitaji ya udhibiti wakati wa kutoa huduma za malipo ya kisasa.

Naye Makamu Rais na Meneja Mikakati wa kampuni hiyo, Mihayo Wilmore, alisema leseni hiyo mpya inaipa kampuni uwezo wa kufanya kazi ndani ya mfumo ikolojia wa fedha wa Tanzania.

Alisema Airpay inajenga makao makuu ya Afrika yenye hadhi ya kimataifa visiwani Zanzibar sambamba na mpango wa Silicon Zanzibar.

Wilmore alisema wanaishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mtazamo wake wa dira na kuweka vipaumbele vya kidijitali, akisema huduma za malipo za Airpay zimejitolea kudumisha viwango vya juu vya usalama.

Alisema Airpay ni kampuni ya kwanza ya kutoa huduma za fedha ya India iliyojumuisha huduma za kifedha za aina mbalimbali inayowawezesha watumiaji, wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo katika mkondo wa mwisho wa huduma.

Alisema kampuni hiyo imewezesha uwepo wa watumiaji wadogo katika vijiji zaidi ya 5,900 India, unaojumuisha wilaya 558, majimbo 37 na wajasiriamali wadogo zaidi ya 500,000.

# Maofisa habari, waandishi wahimizwa kufahamu teknolojia za mawasiliano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Habari Maelezo Zanzibar, Hassan Khatib, amewataka maofisa habari na waandishi wa habari kuwa na uelewa wa kina wa teknolojia za mawasiliano na vyombo vya habari vya kisasa, ili kutoachwa nyuma na kasi ya sayansi na teknolojia.

Aliyasema hayo wakati akisoma hotuba ya Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Sanaa na Michezo Zanzibar, Fatma Rajabu Hamad, wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari na maofisa habari na mawasiliano yaliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya UNESCO Tanzania.

Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha uwezo wa maofisa habari na wanahabari katika kutoa taarifa za serikali kwa wananchi kwa uwazi na kufundisha umma kutumia fursa za teknolojia za kisasa katika upatikanaji wa habari.

Mkurugenzi huyo alisema ni muhimu sana kwa wanahabari kuwa na uelewa wa kina wa teknolojia za mawasiliano na vyombo vya habari vya kisasa ikiwemo mitandao ya kijamii na majukwaa mengine ya kidijitali yanavyofanyakazi.

"Kutokana na kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, jamii imekuwa na wigo mpana wa kupata taarifa nyingi na kwa haraka"alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ni muhimu sana kwa waandishi na maofisa wa habari kuwa wabunifu katika mawasiliano yao na umma ili maudhui yao kueleweka kwa urahisi na kuwavutia watu wanaowalenga.

Aidha, aliwataka maofisa habari kujenga uhusiano mzuri wa kikazi baina ya vyombo vya habari, wadau na umma lakini pia wanapaswa kufahamu, njia za kisasa za mawasiliano zimerahisisha pia upatikanaji wa taarifa zisizokuwa sahihi.

"Kama kuna matokeo hasi kwenye njia za kisasa za mawasiliano basi upotoshwaji wa taarifa ni moja kati athari hasi. Wengine wanasema hizi ni enzi za habari feki. Hivyo maofisa wa habari wanatakiwa kuwa makini na kuhakikisha kuwa wanatoa habari sahihi na za kuaminika" alisema.

Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa UNESCO, Aboud Khamis, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha uwezo wa maofisa habari na waandishi wa habari katika kutoa taarifa na kuhabarisha umma, kutumia fursa za teknolojia za kisasa katika upatikanaji wa habari.

Alisema kupitia mafunzo hayo maofisa habari na mawasiliano, wataongezewa maarifa katika kufanyakazi ambazo zitaleta tija kitaifa na kimataifa.

Naye Mkufunzi wa masomo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Imane Duwe, aliwataka maofisa habari kuwa wabunifu na kwenda na kasi ya teknolojia ili kazi zao kutambulika kwa haraka katika kutoa taarifa.




Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, akizungumza katika mkutano mkuu wa majimbo ya Mtambwe, Wawi, Wingwi na Kiwani kisiwani Pemba, wakati wa kuhitimisha ziara yake ya kukagua uhai wa chama juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushirikiano Tanzania, China wamkosha Dk. Mwinyi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameishukuru Serikali ya China kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa kwa Tanzania, ikiwemo Zanzibar kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo.

Alitoa shukurani hizo Ikulu Zanzibar, wakati akiwakabidhi vyeti na medali timu ya madaktari 32 kutoka China waliotoa huduma za matibabu kwenye hospitali za Zanzibar kwa kipindi cha mwaka mmoja na kuwaaga baada ya kumaliza muda wao nchini.

Rais Dk. Mwinyi alisema, Zanzibar imenufaika na fursa nyingi kutoka China kupitia sekta za maendeleo ikiwemo afya na kupokea timu za madaktari bingwa wanaofika nchini kubadilishana uzoefu na wazawa, hali aliyoieleza imeimarisha uhusiano mwema uliopo baina yao pamoja na kujifunza uzoefu wa masuala ya afya.

Dk. Mwinyi alisema Serikali ya Zanzibar imeendeleza maeneo mengi ya afya kwa kujenga hospitali zenye vifaa tiba vya kisasa, kuboresha miundombinu na kuongeza hospitali za wilaya na mikoa pamoja na kuifanyia matengenezo makubwa Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alishukuru kazi kubwa iliyofanywa na madaktari hao kwa kipindi chote walichohudumu Zanzibar akisema serikali inajivunia sana kuwepo kwao.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema ushirikiano uliopo baina ya China na Zanzibar umedumu kwa miaka 60 sasa na China ikiisadia Zanzibar kimaendeleo hasa katika sekta ya afya. Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Amour Suleiman Mohammed, alisema timu hiyo ya madaktari bingwa kutoka China iliwasili nchini Septemba 26 mwaka 2022 na Septemba 26 mwaka huu inatarajiwa kurejea nchini kwao.

Alisema timu hiyo ilitoa msaada wa kitabibu kwa wananchi wa Unguja na Pemba kwa magonjwa ya macho, meno, mkojo, figo, huduma za X- ray, pia ilifanya upasuaji kwa wagonjwa zaidi ya 50 kwa maradhi tofauti.

Kiongozi mkuu wa timu ya madaktari hao , Dk. Zhao Xiaojun, aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano ilioutoa kipindi chote na kueleza Zanzibar ni visiwa vyenye upendo, amani na mshikamano kwa wenyeji na wageni.

# Mkutano wa 12 Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuanza leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa 12 wa Baraza la 10 la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza leo Chukwani visiwani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu wa baraza hilo, Raya Issa Mselem, alisema katika mkutano huo kutakuwa na shughuli mbalimbali za baraza ambazo zitafanyika ikiwemo maswali na majibu 116.

Aidha, alisema kutawasilishwa ripoti za wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati za Kudumu za Baraza kwa mwaka 2022/2023.

Katibu huyo alisema kuwa pia kutakuwa na ripoti ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC).

Alisema taarifa nyingine itakayowasilishwa ni taarifa ya Serikali kuhusu ripoti ya jitihada za utekelezaji wa kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar mwaka 2022.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIZABETH C. SINO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index number **S1144-0528** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ISIMILA SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHU/RB/269303/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER HUMPHREY TERRY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI ESCUDO yenye usajili namba **T 692 AYP,** CHASSIS NAMBA: **TD01W150749** na ENGINE NAMBA: **G16A358615.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/ARU/2069/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAPPY WILSON ELISHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **TVS KING** yenye usajili namba: **MC 822 BSE.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**M/TR/RB/496/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DEOGRATIUS PETER KAMNDE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA** yenye jina la umiliki AL **BRASHIDI TRADING** yenye usajili namba **T 333 ART,** CHASSIS NAMBA: **AE1107003562** na ENGINE NAMBA: **5AB958713.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/ARU/2121/203**

## KUPOTEA KWA YA GARI

**ARK GENERAL BUSINESS LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISH CANTER** yenye usajili namba **T597 DSG.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DOD/DOD/2486/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Titus Mgese Mayuma** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki **MC 266 CYR** aina ya Kinglion. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Titus kwa simu namba **0629871627.**

Taarifa ya Polisi:

**MGZ/RB/859/2023.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 103 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MATONYA CHIWALIGO of MNYAKONGO NKUHUNGU within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MARY MATONYA CHIWALIGO**

**GENERAL CITATION
(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admirations made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 day of 09, 2023.

**Date at Dodoma this 9th Day of August, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE I/c DODOMA DISTRICT

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA KINONDONI
MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 193 LA 2023**

1) **BERNARD DOTTO MASUA**
2) **DOTTO MASUA.................. MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SUPERIOR FINANCING SOLUTION...........MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**SUPERIOR FINANCING SOLUTION**

**POPOTE ULIPO/MLIPO:
BERNARD DOTTO MASUA**

**DOTTO MASUA** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 27/09/2023 saa 03:00 Asubuhi/Mchana mbele ya **Mh. J.W. SILLAS.** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 08 Mwezi wa 09/2013

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA MOROGORO
LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 89 YA 2023**

**DENIS D. NTYANGIRI..................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**CONSOLATHA MAGWIRA..................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA
CONSOLATHA MAGWIRA**

POPOTE ULIPO Unaarifiwa Ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro, tarehe 05/10/2023 mbele ya mwenyekiti M. Khasim wewe mwenyewe binafsi au mtume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hutahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 07 mwezi Septemba, 2023.

M. KHASIM
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA MOROGORO, LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI NAMBA 20 YA 2023**

**JUMA HASSANI LUGENDO: ......................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MWENYEKITI WA SACCOSS HEMBETI
LENIA ANDREW MDAKWA**

**ZUHURA SHABANI: ........................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA
ZUHURA SHABANI**

**POPOTE ULIPO** Unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya Morogoro tarehe 15/09/2023 mbele ya Mwenyekiti E.Mogasa ninyi Wenyewe binafsi au mtume wawakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepang-wa kutajwa.Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi

Imetolewa kwa MKONO wangu na MHURI wa Baraza leo tarehe 08 mwezi September,2w0.

E. MOGASA
MWENYEKITI

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 92/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU JOEL MWENDAMAKA wa HAZINA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**NA DAVID JOEL MWENDAMAKA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 09 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 11 Mwezi **09 Mwaka 2023.**

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI
Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 61/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU ISMAIL RAMADHANI MALENDA wa DODOMA
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA PEACE GODWIN MASASI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 10 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 11 Mwezi 09 Mwaka 2023.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na. 1323/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU AGATHA MAX PUPA wa DAR ES SALLAM
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA MARIA YOHANA PUPA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 09 Mwaka 2023 saa 2 asubuhi kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Imetolewa leo Tarehe 06 Mwezi 09 Mwaka 2023.

HAKIMU

---

**TAOMTRA LIMITED**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA TANGA**

**TANGA SHAURI LA NDOA NAMBA 13/2022**

**AMINA SELEMANI NJAMA ...........................MSHINDA TUZO**

**DHIDI YA**

**SALUM HAMISI YAMLINGA.........................MSHINDWA TUZO**

**TAOMTRA Limited** kwa Idhini na Mamlaka tuliyopewa na Mahakamaya Mwanzo Wilaya ya Tanga kupitia maombi Na.13/2022 tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba moja iliyopo Pongwe wilaya ya Tanga. Mnada utafanyika 25/09/2023 saa nne asubuhi mahali nyumba ilipo.

**MASHARTI YA MNADA**

1. Nyumba itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atakaeshinda atalipa malipo ya awali ya 25% au zaidiya bei itakayofikiwa siku ya mnada na 75% katika muda wa siku 14.
3. Mnunuzi akishindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyengine itakayopangwa.
4. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua Nyumba kuanzia Tarehe ya Tangazo mpaka siku ya mnada.

**MAWASILIANO**
**TAOMTRA LIMITED S.L.P 02, SINGIDA**
**SIMU: 0627 424 164, 0759 650 037 AU 0785 100 215**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie*

***0745 700 710.***

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Ukraine yatwaa mitambo ya kuchimba gesi

**KYIV,** Ukraine

UKRAINE imesema imefanikiwa kutwaa tena udhibiti wa maeneo manne ya kuchimba gesi kaskazini mwa Bahari Nyeusi, karibu na Peninsula ya Crimea.

**Russia ilitwaa udhibiti wa jengo linaloitwa Boyko Towers mwaka 2015, muda mfupi baada ya kuliteka Crimea kinyume cha sheria.**

Video ya operesheni hiyo ambayo Ukraine inasema ilifanyika mwezi uliopita, ilionyesha vikosi maalumu vikiondoa zana za kijeshi za Russia katika eneo hilo.

Aidha, ilielezwa kuwa Russia ilitwaa udhibiti wa jengo linaloitwa Boyko Towers mwaka 2015, muda mfupi baada ya kuliteka Crimea kinyume cha sheria.

Video na taarifa iliyotolewa na idara ya ujasusi ya kijeshi ya Ukraine, yenye jina 'Battle for the Sea' inatoa taswira adimu katika nyanja hii ya mzozo.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa katika video hiyo, ambayo BBC haikuweza kuithibitisha, ilionyesha boti ngumu zilizoonekana zikivuka Bahari Nyeusi, zikiwa zimebeba timu za vikosi maalumu vya Ukraine.

Wakati mmoja, boti hizo hupita karibu na Kisiwa cha Snake, kinachojulikana pia kama Kisiwa cha Zmiinyi, ambacho kilitekwa na Russia katika siku ya kwanza ya uvamizi wake kamili mwaka jana na kukamatwa tena miezi minne baadaye.

Pia taarifa ya Ukraine ilieleza kuwa wanajeshi walionekana wakipanda kwenye eneo moja la uchimbaji gesi na kuondoa vifaa vya Russia, pamoja na vifaa muhimu vya rada.

"Kwenye maeneo ya kuchimba visima, Warassia waliweka maghala yenye risasi na mafuta ya helikopta, pia waliweka vituo vya rada kwenye minara kwa usaidizi ambao walifuatilia hali katika Bahari Nyeusi," ilisema. **BBC**



Maandamano yaliyofanyika mjini Jerusalem nchini Israel dhidi ya mageuzi ya mfumo wa mahakama, jana. **PICHA: REUTERS**

# Israel yakabiliwa na mgogoro wa kikatiba

**JERUSALEM,** Israel

ISRAEL imeingia katika mgogoro wa kikatiba baada ya mageuzi ya mfumo wa mahakama yanayotarajiwa na serikali ya mrengo wa kulia wa Benjamin Netanyahu, kutajwa kuchochea mgogoro mkubwa wa kitaasisi na maandamano ya mara kwa mara.

Inaelezwa kuwa katika taifa hilo kumeshuhudiwa maandamano ya wananchi, mgogoro ambao haujawahi kushuhudiwa unaoripotiwa kati ya serikali na upande mmoja na Mahakama ya Juu.

Mahakama ya Juu nchini humo inachunguza kubatilishwa kwa sheria iliyopitishwa mwezi Julai mwaka huu, sheria inayonuiwa kuzuia mamlaka yake.

Israel inazidi kutumbukia katika mzozo hadi kufikia hatua ya kujikuta kwenye hatihati ya mgogoro wa kikatiba. Ikibainishwa kuwa demokrasia ya Israeli inategemea kanuni ya kugawana madaraka, utendaji, utungaji sheria na mfumo wa mahakama yaani serikali, Bunge na Mahakama ya Juu.

Inaelezwa kuwa kwa serikali na Bunge, Mahakama ya Juu ya Israeli ina nguvu zaidi. Na kwamba mwanzoni mwa mwaka huu, walizindua mageuzi ya mfumo wa mahakama, ambayo yanalenga kuzuia mamlaka ya mfumo wa mahakama.

Inabainishwa kuwa kutokana na mswada huo, Serikali ya Israel inataka kupitia upya mamlaka ya Mahakama ya Juu. Na kwamba inataka kujumuisha kifungu ambacho kitawezesha Bunge, kwa kura nyingi, kubatilisha uamuzi wa Mahakama hiyo. **RFI**

# ECOWAS yakabiliwa na mtihani

**AFRIKA MAGHARIBI**

MSURURU wa mapinduzi katika mataifa ya ukanda wa Afrika Magharibi unaweka umoja na uwezo wa Jumuiya ya Kikanda ya (ECOWAS), katika mtihani, licha ya kujaribu kurejesha utawala wa kiraia katika nchi kama Burkina Faso, Guinea, Mali na Niger.

Mataifa hayo manne yameungana kupinga vikwazo vya kiuchumi, na hatua zinazoweza kuchukuliwa za kijeshi, na nchi zingine 11 wanachama wa jumuiya hiyo. Huku wataalam wakionya uwezo wa ECOWAS kushughulikia changamoto za kiusalama unaohatarishwa na kuongezeka kwa viongozi wapya wa kijeshi.

Inaelezwa kuwa jumuiya hiyo ya kiuchumi ya mataifa ya Afrika Magharibi inatatizika jinsi ya kukabiliana na utawala wa kijeshi nchini Niger, ambao umekuwa madarakani kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa.

Moja ya sababu zinazotajwa za mapinduzi hayo ni madai ya utawala mbovu unaosimamia vibaya rasilimali za nchi na kuruhusu hali ya usalama kuzorota.

Ilielezwa kuwa mizozo ya kisiasa na kiusalama inayoendelea nchini Niger, Burkina Faso, Guinea, na Mali inaonekana kuwa changamoto kwa nchi nyingine 11 wanachama wa ECOWAS.

Paul Melly, mshauri wa masuala ya Afrika katika taasisi ya Chatham House, mjini London, alisema viongozi wa mapinduzi hawazingatii masharti yaliyowekwa na ushirikiano wa jumuiya hiyo ya kikanda.

"Msururu huu wa mapinduzi, ni pigo kubwa sana kwa kile kilichokuwa nguvu kuu ya ECOWAS. Na ukweli kwamba tawala za kijeshi zinakaidi utamaduni wa muda mrefu wa ECOWAS wa kushirikiana katika kuweka kanuni za utawala, na katika kudhibiti mizozo ni tishio la kweli, na ni changamoto kwa umoja wa kikanda," alisema.

Mnamo mwaka wa 2017, ECOWAS ilisifiwa kwa hatua yake ya kijeshi ya pamoja dhidi ya Rais wa Gambia Yahya Jammeh, na kumlazimisha kujiuzulu baada ya kushindwa katika uchaguzi wa rais wa sasa, Adama Barrow.

Francis Mangeni, mtaalam wa utangamano wa kikanda, alibainisha kuwa hali ya sasa ni tofauti kabisa, huku baadhi ya mapinduzi yakiungwa mkono na wananchi.

"Sasa tuko katika hali ambayo haiko wazi, watu wenyewe wanaunga mkono mapinduzi. Kwa hiyo hii inaleta aina fulani ya changamoto, kwa maneno mengine, uhalali wa serikali iliyochaguliwa kikatiba unaonekana kuwa katika shaka.

"Na hili ni jambo la ajabu kusema kwa sababu ikiwa serikali ni za kikatiba, zinapaswa kuwa halali, lakini inaonekana watu hawafikirii hivyo," alisema.

Vilevile, inaelezwa kuwa viongozi wa Umoja wa Afrika (AU) wamekuwa wepesi kuwashutumu wakuu wa nchi wanaobadilisha katiba ili kuongeza muda wao wa kukaa madarakani na kubadilisha ukomo wa umri ili kubaki madarakani.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, kuongezeka kwa utekaji wa kijeshi barani Afrika unatokana na viongozi kukatalia kwenye madaraka, dosari katika uchaguzi, na viongozi waliochaguliwa kushindwa kufanya kazi kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi. **VOA**

# EMIRATES YANOGESHA HAMASA KOMBE LA DUNIA RUGBY 2023

**Dubai,** UAE

KAMA mshirika wa Kimataifa wa Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby 2023 (RWC 2023), Kampuni ya Emirates imezindua kampeni ya mashindano hayo yenye thamani kubwa kwa video ya kucheza inayomwonesha mwamuzi maarufu wa Afrika Kusini, Jaco Peyper.

Kampeni hiyo inajumuisha video yenye furaha ambayo inamuonesha Jaco akiongoza ndege ya Emirates A380 yenye nembo maalum ya RWC 2023 kwenye uwanja wa ndege, tayari kwa kuruka huku akikimbia mbele ya ndege na kupuliza filimbi kuashiria kurushwa.

Ndege ya Emirates A380 basi, inaruhusiwa kuruka, ikielekea Paris, Ufaransa kuanza Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby 2023.

**Video yenye kuchekesha inafuata mafanikio ya safu ya iliyoshinda tuzo ya 'Whistle Watch', safu iliyotolewa na World Rugby iliyoongozwa na mwamuzi wa zamani wa Kimataifa Nigel Owens na kudhaminiwa na Emirates.**

Kupitia mashindano hayo, mashabiki wa mpira wa rugby wanaweza kutarajia vipindi maalum vilivyorekodiwa nchini Ufaransa.

Emirates inafurahia uwapo mkubwa wa nembo wakati wa mashindano, ikiwa ni pamoja na nembo ya Msimamizi wa Televisheni, pamoja na haki za ukarimu na tiketi.

Ndege pia itazindua eneo la kuhamasisha mashabiki mwaka huu huko Paris, Lyon, na Marseille na mipango ya kufurahisha "kuruka vema zaidi". Wafanyakazi wa Emirates Cabin Crew watapiga picha kumbukumbu maalum kwa mashabiki wa mpira wa rugby na kamera ya papo hapo, iliyochapishwa kwenye fremu maalum ya picha ya RWC 2023.

Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby ni moja ya matukio makubwa na maarufu zaidi ulimwenguni, likifanyika mara moja kila baada ya miaka minne. Mwaka huu, mashindano hayo yalianza Septemba 8 na yatamalizika Oktoba 28, mwaka huu ambapo yanaendelea katika miji tisa nchini Ufaransa. Jaco ndiye aliyepuliza kipenga siku ya ufunguzi ya Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby 2023 kati ya mwenyeji, Ufaransa na New Zealand kwenye Uwanja wa Stade de France (Saint-Denis).

Ushirikiano wa Emirates na World Rugby ulianzia mwaka 2007 wakati shirika hilo la ndege lilianza kuwa mdhamini wa Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby 2007 nchini Ufaransa.

Baada ya hapo shirika hilo la ndege likawa Mshirika wa Kimataifa wa Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby 2011 huko New Zealand na Mshirika wa Kimataifa wa kwanza kusaini makubaliano kwa Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby la England 2015 na Japan 2019 na sasa Ufaransa 2023 huku pia likiwa tayari tena kwenye Kombe la Dunia la Mpira wa Rugby la Australia 2027. Emirates pia ni mdhamini wa Maafisa wa Mpira wa Rugby na waamuzi bora zaidi.

KIPUTE...



Wachezaji wa timu za soka ya Kewanja FC na Mrito FC, wakichuana vikali katika mechi ya fainali ya mashindano ya Kemanyanki Cup iliyofanyika Nyamongo, Tarime jana, kwa udhamini wa Barrick North Marana. Kewanja FC iliibuka mshindi kwa kuichapa Mrito FC kwa mikwaju yapenati 4-2. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shabiki Yanga ashinda mil. 120/-

**Na Mwandishi wetu**

SHABIKI wa Klabu ya Yanga, Paulo Martin, ameshinda Sh. 120,989,610 za Tanzania baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali duniani kupitia mchezo wa Perfect 12 wa Kampuni ya M-Bet.

Martin ambaye ni mwanajeshi na mjasiriamali, alikabidhiwa fedha zake na Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, katika hafla fupi iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Mushi alisema Martin anaungana na washindi wengine mbalimbali ambao wameshinda mamilioni kupitia droo ya Perfect 12 na kubadilisha maisha yao.

"Martin anakuwa mmoja wa wanachama wa nyumba yao ya mabingwa ambao kwa sasa imesheheni mamilionea mbalimbali. Tunaposema M-Bet ni nyumba ya mabingwa, tunakuwa na maana maalum, mpaka sasa tumewazawadia mamilioni washindi mbalimbali," alisema Mushi.

Alisema M-Bet itaendelea kubadilisha maisha ya Watanzania kupitia michezo yake mbalimbali ya kubashiri na kuwaomba watu wenye umri kuanzia miaka 18 kushiriki.

"Kubashiri si kazi, naomba watu wajue, ni burudani ambayo inakufanya kuibuka milionea endapo utashinda, M-Bet inajisikia fahari sana kuendelea kuwatoa washindi na kubadili maisha yao," alisisitiza Mushi.

Kwa upande wake, Martin alisema alianza kubashiri miaka mitatu iliyopita na anashukuru ndoto zake kutimia.

"Nimeanza kubashiri kupitia M-Bet na sijahama kwa sababu ni kampuni ambayo imekuwa ikitangaza washindi wengi. Nimeona washindi wengi na nikaamini kuwa ipo siku na mimi nitakuwa natangazwa kuwa mshindi. Ndoto yangu imetimia. Nitatumia fedha hizo kwa kuendeleza biashara zangu na shughuli nyingine za kimaendeleo," alisema Paulo.

# Simba SC, Yanga zaungana kuisapoti Singida CAF

**Na shufaa Lyimo**

KUELEKEA mechi ya raundi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Future FC ya Misri, Klabu Kongwe nchini, Simba na Yanga, zimeungana pamoja kutoa hamasa kwa wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano hiyo, Singida Fountain Gate FC.

Singida FG Jumapili wiki hii itaikaribisha Future FC katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kabla ya timu hizo kurudiana nchini Misri baada ya wiki mbili na mshindi wa jumla atafuzu moja kwa moja hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Hata hivyo, ili kuhakikisha Singida FG inasonga mbele mashabiki wengi hususan wa Simba na Yanga wametakiwa kujitokeza kwa wingi katika mchezo huo Jumapili, Maafisa Habari wa klabu hizo pamoja na wa Azam FC, wameungana kutoa hamasa kwa wapenzi wa timu zao kwa kuwataka kuwa nyuma ya Singida FG siku hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Klabu ya Singida Fountain Gate, Hussein Masanza, alisema lengo la kuunda umoja huo ni kuhakikisha timu yao inafanya vema na kuweza kusonga mbele.

"Tumeamua kuunda umoja huu kwa lengo la kuipa sapoti timu yetu, tumefanya maandalizi ya kutosha ambayo yataisaidia timu yetu kusonga mbele," alisema Masanza.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Yanga,

Ali Kamwe, alisema Kocha wao Mkuu, Miguel Gamondi ametoa mifumo mitatu itakayowasaidia timu ya Singida Fountain Gate kuifunga Future FC.

"Gamondi ametoa mifumo mitatu kwa ajili ya kumkabidhi Kocha Mkuu wa Singida Fountain Gate, itakayomsaidia kupata matokeo mazuri, ninaomba Watanzania waje kwa wingi kuisapoti timu hii," alisema Kamwe.

Wakati Kamwe akichagiza kwa kauli hiyo, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria 'Zaka za Kazi', aliwataka Watanzania kuungana pamoja kuisapoti timu hiyo na kuachana na mambo ya ushabiki.

"Tunapaswa kuungana pamoja ili tuhakikishe timu hii inapata ushindi na kuweza kusonga mbele," alisema Zaka za Kazi.

Hata hivyo, kwa upande wa Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, hakuweza kutokea katika mkutano huo na wanahabari baada ya kuomba udhuru kuwa yupo mahakamani, lakini Masanza alisema wapo pamoja katika kuiunga mkono Singida FG kuelekea mechi hiyo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### SANCHO KUONDOKA UNITED

WINGA wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, atataka kuondoka Manchester United baada ya mazungumzo na kocha Erik ten Hag kueleweka kuwa yamesababisha wawili hao kushindwa kusuluhisha tofauti zao. (Star)

#### EL GHAZI AFIKIRIWA UTD

KLABU ya Manchester United inafikiria kumnunua winga wa zamani wa Ajax, Aston Villa na Everton, Anwar El Ghazi, huku Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 28, akiwa mchezaji huru baada ya kuondoka PSV Eindhoven. ***(Mail)***

#### NAGELSMANN ATAJWA

KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann na kocha wa zamani wa Uholanzi, Louis van Gaal, wako kwenye orodha fupi ya kumrithi Hansi Flick aliyetimuliwa kama kocha wa Ujerumani. ***(Mirror)***

#### GABRIEL AITULIZA ARSENAL

MLINZI wa Arsenal, Gabriel alipunguza hofu kwamba anaweza kujeruhiwa baada ya kufanya mazoezi na wachezaji wenzake wa Brazil, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, akitoka katika ushindi wa nchi yake dhidi ya Bolivia Ijumaa iliyopita. ***(Standard)***

#### VAN GAAL AHOFU NAFASI

KOCHA wa zamani wa Manchester United, Luis Van Gaal alisema "naheshimika" kuhusishwa na wadhifa wa ukocha wa Ujerumani, lakini akaongeza "hakuna mgeni aliyewahi kuteuliwaa kwa wadhifa wa ukocha nchini Ujerumani". ***(Sky Sports Germany)***

#### NAGELSMANN NAFASI KUBWA

JULIAN Nagelsmann anachukuliwa kuwa kipenzi cha nafasi hiyo, lakini bado ana mkataba na Bayern Munich, ambao wanaweza kuiomba FA ya Ujerumani ada ya kumnunua kocha huyo mwenye umri wa miaka 36. ***(Bild)***

#### MAGATH AJIPIGIA DEBE

KOCHA wa zamani Bayern Munich na Fulham, Felix Magath anaamini anazo sifa za kuwa meneja wa Ujerumani. ***(Sky Sports)***

#### WALKER, KUSTAAFU ENGALND

KOCHA wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, amesema alizungumza mara mbili na beki, Kyle Walker kuhusu kustaafu kimataifa. Beki huyo wa Manchester City mwenye umri wa miaka 33, alifikiria kustaafu England baada ya Euro 2020 na Kombe la Dunia 2022, lakini akashawishiwa kuendelea. ***(Mail)***

#### LAVIA AIPA PIGO CHELSEA

CHELSEA inahofia kiungo mpya aliyesajiliwa Romeo Lavia, 19, atakuwa nje kwa wiki sita baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kuumia kifundo cha mguu wakati wa mazoezi. ***(Mirror)***

#### ARSENAL KWA DIOMANDE

ARSENAL walikuwa na ofa ya pauni milioni 30 kwa ajili ya mlinzi wa Sporting CP, Ousmane Diomande mwenye umri wa miaka 19, na ilikataliwa msimu wa majira ya joto, lakini watajaribu kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwakani. ***(Record, via Metro)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA HATARINI KUTUPWA JELA YA SOKA MIAKA MINNE

**TURIN,** Italia

KIUNGO wa kati wa Juventus, Paul Pogba, anakabiliwa na hatari ya kufungiwa kucheza soka kwa miaka minne, baada ya kupimwa na kukutwa ametumia dawa za kusisimua misuli zilizopigwa marufuku, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

**Shirika la kupambana na dawa za kusisimua misuli la Italia lilitangaza Jumatatu kwamba, vipimo hivyo vilifanywa baada ya mechi ya Juventus dhidi ya Udinese Agosti 20, mwaka huu.**

Pogba hakucheza mechi hiyo ya Serie A, lakini alikuwa kwenye benchi la Juventus.

Nado Italia, wakala wa kukabiliana na matumizi ya dawa za kusisimua misuli, ilieleza kuwa Pogba amesimamishwa kwa muda.

Kwa sasa anasubiri vipimo vya sampuli na iwapo atakutwa na hatia anaweza kusimamishwa kucheza soka kwa kipindi cha hadi miaka minne.

"Mwendesha mashtaka wa kitaifa wa kupambana na dawa zilizokatazwa michezoni, ametoa nafasi ya kusimamishwa kwa muda kwa mwanamichezo, Paul Labile Pogba," Nado Italia ilisema katika taarifa yake.

Mahakama hiyo ilisema Pogba alikiuka sheria za kupinga matumizi ya dawa za kusisimua misuli na kuongeza kuwa matokeo "yaliendana na yalionesha alitumia dawa hizo."

Juventus ilitoa taarifa ikikubali matokeo chanya na kusimamishwa na kuongeza kuwa "tutatathmini hatua zinazofuata za kiutaratibu."

"Tunasubiri matokeo ya uchambuzi na hatuwezi kusema lolote hadi wakati huo," Wakala wa Pogba, Rafaela Pimenta, alisema katika taarifa iliyoripotiwa na vyombo vya habari vya Italia.

"Jambo la uhakika ni kwamba Paul Pogba hakuwahi kukusudia kuvunja sheria."

●●● Tutatathmini hatua zinazofuata za kiutaratibu, tunasubiri matokeo ya uchambuzi...

Ni dokezo lingine hasi kwa mchezaji ambaye amekuwa akisumbuliwa na majeraha tangu ajiunge tena na Juventus kutoka Manchester United zaidi ya mwaka mmoja uliopita.

Aliondolewa kwenye kikosi cha Ufaransa katika fainali ya Kombe la Dunia mwaka jana kutokana na jeraha la goti. Pia kumekuwa na uchunguzi wa polisi unaoendelea nchini Ufaransa kuhusu madai kwamba Pogba alilengwa na wanyang'anyi akiwamo kaka yake mkubwa Mathias, ambaye amekana kufanya makosa yoyote.

Mapema Jumatatu, Pogba alisema alifikiria kustaafu wakati matukio yakiendelea.

Pogba bado hajaanza mchezo wowote msimu huu, lakini amecheza mechi mbili akitokea benchi, mara ya mwisho akicheza katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Empoli.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,152,9

MECHI KALI
FC LUZERN II
VERSUS
BREITENRAIN
1 | 1.60
X | 4.14
2 | 4.14

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Fatuma Kinokela - 0653 528 XXX
2. Respikius Stanslaus - 0656 077 XXX
3. Maria Mlenga - 0659 474 XXX
4. Orijia Tibaza - 0676 548 XXX
5. Samora Leguna - 0710 647 XXX
6. Amos Mgombera - 0712 194 XXX
7. Vicent Jidayi - 0712 414 XXX
8. Hafidhi Maulid - 0713 091 XXX
9. Rashidi Njiku - 0719 335 XXX
10. Joseph Masine - 0779 977 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# TEN HAG KUAMUA HATIMA YA SANCHO




**MANCHESTER,** England

JADON Sancho yuko tayari kwa mazungumzo na kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, vyanzo vimeiambia ESPN kutokana na mzozo kati ya wawili hao baada ya kufungwa mabao 3-1 na Arsenal.

Sancho alirejea Carrington Jumatatu pamoja na wachezaji wengine ambao hawajahusika katika mechi wakati wa mapumziko ya kimataifa.

Itakuwa ni mara ya kwanza kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kukutana ana kwa ana na Ten Hag baada ya uamuzi wake wa kukanusha hadharani madai yaliyotolewa na Mholanzi huyo kwamba alitemwa kwenye mechi ya Arsenal kwa sababu ya kufanya vibaya mazoezini.

Katika chapisho la mtandao wa kijamii ambalo bado liko mtandaoni, Sancho alisema "si kweli kabisa, nimefanya vizuri sana kwenye mazoezi."

Ten Hag anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wa Sancho baada ya mazungumzo na winga huyo wa zamani wa Borussia Dortmund.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Man United itaunga mkono chochote ambacho Ten Hag atakiamua.

Chanzo kutoka ndani ya Man United kiliiambia ESPN kwamba hatima ya Sancho itaamuliwa bila ya sababu zingine zozote, pamoja na likizo ya Antony.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil, Antony amepewa muda na klabu hiyo huku kukiwa na madai ya unyanyasaji aliofanywa kwa wanawake watatu na hakuna muda wa kurudi kwake.




## Klopp atajwa ukocha Ujeruman

**BERLIN,** Ujerumani

SHIRIKISHO la Soka la Ujerumani (DFB), linamchukulia Jurgen Klopp kuwa mmoja wa wagombea wakuu kuchukua nafasi iliyo wazi ya kocha mkuu wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, kwa mujibu wa 90min.

Hansi Flick amekuwa kocha wa kwanza wa Ujerumani kuwahi kufutwa kazi mapema zaidi kutokana na kipigo kibaya cha mabao 4-1 kutoka kwa Japan Jumamosi iliyopita.

Flick alikuwa amesimamia kampeni ya kukatisha tamaa ya Kombe la Dunia, ambapo Ujerumani ilishindwa na kutolewa katika hatua ya makundi na kucheza michezo mitano bila ushindi tangu Machi mwaka huu.

Kuelekea kwenye michuano ya Euro 2024 msimu ujao wa majira ya joto, Ujerumani sasa wamembadilisha Flick na kumchukua kocha wa kiwango cha juu, na vyanzo vimethibitisha kwa 90min kwamba Klopp anachukuliwa kuwa mmoja wa chaguo lao kuu kwa nafasi hiyo iliyo wazi.

DFB wamevutiwa sana na Klopp na wanafikiria kumpa kazi hiyo kwa muda wote kabla ya Euro 2024.

Katika mahojiano na
Germany wakati wa
jira ya joto, Klopp aliuli
kuhusu uwezekano wa
chukua kazi Ujerumani, s
ambalo alijibu hivi: "Kaz
ukocha wa timu ya taifa
kuwa heshima kubwa - ha
na swali kuhusu hilo. Ta
ambalo linazuia mambo y
ni uaminifu wangu.

"Siwezi kuondoka
erpool sasa na kusema
taichukua Ujerumani
muda mfupi. Hilo halif
kazi na ombi halipo. Ik
nitatakiwa kufanya h
wakati fulani, basi laz
niwe huru na kwa sasa ha
na, nina jukumu na klabu

911,993/-

# MWAKINYO ATAMBA KUMCHAKAZA MKENYA UBINGWA IBA SEPTEMBA

Na Saada Akida

KUELEKEA pambano lao la kuwania mkanda wa Ubingwa wa Mabara (IBA), Bondia wa Ngumi za Kulipwa Tanzania, Hassan Mwakinyo, amesema amejipanga vizuri baada ya kumsoma mpinzani wake, Rayton Okwiri kutoka Kenya.

Mwakinyo juzi alipima afya ikiwa ni ishara ya kuwa tayari kwa pambano hilo linalotarajiwa kufanyika Septemba 29, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

**Akizungumza na Nipashe jana, Mwakinyo alisema amejiandaa vizuri kuelekea pambano hilo dhidi ya Mkenya huyo lengo likiwa ni kuhakikisha anampiga mapema.**

Alisema kwa sababu ya kumsoma vizuri mpinzani wake huyo na maandalizi aliyoyafanya, anaimani siku hiyo itakuwa ya taifa kwa kuhakikisha anaipeperusha vema bendera ya Tanzania.

"Siku hiyo itakuwa Sikukuu ya Taifa kwa sababu nimejiandaa vizuri, lakini nimeona mapambano ya mpinzani wangu ninayekwenda kucheza naye, si bondia mbaya, ila ninaimani utakuwa mchezo mzuri," alisema.

Alisema pambano litakuwa zuri na kwamba hakuna shabiki ambaye atahuzunika kutokana na mbinu nyingi alizokuwa nazo katika kumshambulia mpinzani wake huyo.

"Awali nilitakiwa kupigania Mkanda wa WBO ambao (hata hivyo) imeshindikana kuwania kwa sababu ya masharti ya mikanda hiyo, sasa nimepata pambano hili, niwahakikishie Watanzania kuwa sitakubali kupoteza Mkanda wa IBA," alisema Mwakinyo.




Mchezaji wa timu ya Shule ya Sekondari Juhudi, Ali Ahmad, akimiliki mpira huku akizongwa na wacheaji wa timu ya Polisi Kings jana, wakati wa michuano ya vijana ya mpira wa kikapu chini ya umri wa miaka 16, inayoendelea katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Robertinho atamba

INATOKA UKURASA 24

alisema Robertinho.

Alisema kwa ratiba ilivyo wanatarajia kuondoka nchini kesho kuelekea Zambia tayari kwa mchezo huo na watarejea haraka kujipanga kwa ajili ya mchezo wa marudiano ambao utathibitisha timu itakayofuzu hatua hiyo ya makundi.

Kama Simba itafanikiwa kutinga hatua hiyo itakuwa mara ya tano kwenye michuano hiyo tangu msimu wa 2019-2020.

## *Simba, Yanga zapewa maagizo mazito CAF*

INATOKA UKURASA 24

"Tunakumbuka msimu uliopita Yanga aliondolewa kwenye haya mashindano na kwenda shirikisho na kufika fainali, Simba wao waliishia robo fainali ya michuano Ligi ya Mabingwa Afrika, tunatarajia kwa kushirikiana wao basi timu hizi zitafika nusu fainali na fainali," alisema naibu waziri huyo.

Alisema mpira wa miguu Tanzania umezidi kuimarika na timu za taifa zinafanya vizuri ikiwamo Taifa Stars ambayo imefuzu kucheza Afcon, hivyo Simba na Yanga zinatakiwa kukanyagia hapo hapo.

Wawakilishi hao wa Tanzania wanatarajia kuondoka nchini Alhamisi hii, Simba ikielekea nchini Zambia kuwakabili wenyeji wao Power Dynamos huku Yanga wakielekea Rwanda kuvaana na Al-Merrikh.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.16/09/23 | 17:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.41 | 3.25 | 2.80 |
| 02.16/09/23 | 17:00 | Kilmarnock FC vs Hibernian FC | 2.48 | 3.30 | 2.70 |
| 03. 16/09/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs FC Famalicao | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 04. 16/09/23 | 19:00 | Inter Milano vs AC Milan | 2.16 | 3.35 | 3.15 |
| 05. 16/09/23 | 19:30 | VfL Bochum vs Eintracht Frankfurt | 2.80 | 3.50 | 2.27 |
| 06. 16/09/23 | 20:00 | USL Dunkerque vs Grenoble Foot | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 07. 16/09/23 | 20:00 | Rodez Aveyron Football vs Angers SCO | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 16/09/23 | 20:00 | Paris FC vs Amiens SC | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 16/09/23 | 20:30 | SK Sturm Graz vs FC Salzburg | 2.70 | 3.30 | 2.24 |
| 10. 16/09/23 | 21:45 | Cardiff City vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 17/09/23 | 13:30 | Cagliari Calcio vs Udinese Calcio | 2.85 | 3.25 | 2.39 |
| 12. 17/09/23 | 15:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.50 | 2.90 | 2.95 |
| 13. 17/09/23 | 15:30 | FC Twente Enschede vs Ajax Amsterdam | 2.65 | 3.35 | 2.48 |
| 14. 17/09/23 | 16:00 | Frosinone Calcio vs Sassuolo Calcio | 2.75 | 3.35 | 2.40 |
| 15. 17/09/23 | 16:30 | FC Heidenheim vs Werder Bremen | 2.27 | 3.70 | 2.70 |
| 16. 17/09/23 | 17:15 | US Catanzaro vs Parma Calcio | 2.42 | 3.00 | 2.65 |
| 17. 17/09/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs Atalanta BC | 2.35 | 3.45 | 2.75 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 13/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2653 | Chuncheon FC vs Gangneung City | 1.94 | 2.85 | 4.27 |
| 14:30 | 2418 | Wuxi Wuguo vs Suzhou Dongwu | 3.41 | 3.16 | 2.04 |
| 14:30 | 3932 | Jiangxi Liansheng vs Nanjing Fengfan | 6.31 | 4.02 | 1.44 |
| 14:30 | 4113 | Jinan Xingzhou vs Guangzhou Evergrande | 1.65 | 3.56 | 4.69 |
| 14:30 | 4393 | Dongguan Guanlian vs Yanbian Longding | 2.28 | 3.00 | 3.05 |
| 14:30 | 4506 | Anhui Litian vs Shenyang City FC | 1.76 | 3.53 | 4.04 |
| 14:30 | 5822 | Shanghai Jiading Huilong vs Sichuan Jiuniu | 5.48 | 3.45 | 1.59 |
| 14:30 | 5978 | Hebei Kungfu vs Guangxi Pingguo Haliao F.C. | 2.12 | 2.95 | 3.46 |
| 16:00 | 2726 | Hapoel Raanana vs Hapoel Migdal Haemeq | 1.66 | 3.66 | 4.47 |
| 16:40 | 2508 | FC Holon Yirmiyahu vs Hapoel Bikat Hayarden | 2.53 | 3.21 | 2.55 |
| 16:45 | 1854 | Hapoel Kafr Kanna vs FC Tzeirei Kfar Kanna | 2.64 | 3.20 | 2.44 |
| 17:00 | 1272 | MFk Karvina B vs Uhersky Brod | 1.68 | 3.87 | 4.07 |
| 17:00 | 2795 | CA River Plate (Arg) vs Banfield Reserve | 1.68 | 3.25 | 5.08 |
| 17:00 | 3604 | Argentinos Juniors Reserve vs Colon de Santa Fe Reserve | 1.56 | 3.78 | 5.11 |
| 17:00 | 3688 | Estudiantes de LP Reserve vs Newells Old Boys | 2.60 | 3.01 | 2.60 |
| 17:00 | 3751 | Slovacko B vs Blansko | 2.01 | 3.65 | 3.04 |
| 17:00 | 3874 | CA Belgrano vs CA Sarmiento de Junin | 1.69 | 3.46 | 4.58 |
| 17:30 | 3021 | Ironi Nesher vs Hapoel Kaukab | 2.45 | 3.26 | 2.60 |
| 17:30 | 4958 | Fastav Zlin B vs TJ Tatran Bohunice | 1.60 | 4.27 | 4.17 |
| 18:00 | 1587 | Alia Club vs Kfarsoum | 2.20 | 3.20 | 3.00 |
| 18:00 | 3000 | FC Slovan Rosice vs SK Hranice | 1.37 | 4.70 | 6.34 |
| 18:00 | 5399 | Gornik Zabrze II vs Gwarek Tarnowskie Gory | 2.69 | 3.41 | 2.30 |
| 18:45 | 3291 | Sandviken W vs Stabaek W | 1.41 | 4.48 | 5.90 |
| 19:00 | 2371 | Maccabi Y. vs Hapoel Marmorek | 1.74 | 3.31 | 4.48 |
| 19:00 | 4370 | Hlucin vs Start Brno | 1.66 | 4.18 | 3.87 |
| 19:30 | 1481 | Zrinjski Mostar vs NK Posusje | 1.21 | 5.71 | 9.99 |
| 19:45 | 5731 | Ironi Modiin vs Hapoel Herzelia | 2.60 | 3.01 | 2.60 |
| 20:00 | 1946 | SV Heimstetten vs TSV 1860 II | 2.20 | 3.40 | 2.84 |
| 20:00 | 2176 | Valerenga W vs LSK Kvinner W | 1.48 | 4.01 | 5.69 |
| 20:45 | 4018 | Maccabi Ironi Ashdod FC vs Shimshon Kafr Qasim | 1.53 | 3.77 | 5.51 |
| 20:45 | 5699 | Paduano EC RJ vs Perolas Negras RJ | 2.44 | 3.20 | 2.64 |
| 21:00 | 2242 | Circulo Deportivo vs Sol de Mayo | 2.40 | 3.00 | 2.85 |
| 21:00 | 3592 | Dames Zultse Waregem W vs Anderlecht W | 7.94 | 5.50 | 1.26 |
| 21:00 | 3997 | Gimnasia Y Tiro De Salta vs Boca Unidos | 1.57 | 3.36 | 6.10 |
| 21:00 | 4454 | FC Luzern II vs Breitenrain | 1.60 | 4.14 | 4.14 |
| 21:30 | 3329 | Sansinena vs CA Germinal | 1.69 | 3.26 | 4.98 |
| 21:30 | 5286 | Huracan Las Heras vs CSB Atenas | 1.92 | 2.95 | 4.17 |
| 21:30 | 5539 | Sportivo General San Martin vs CA Sol de America de Formosa | 1.65 | 3.26 | 5.30 |
| 21:45 | 2448 | Bala Town vs The New Saints | 6.08 | 4.46 | 1.39 |
| 21:45 | 4654 | Tiverton Town vs Salisbury City | 2.40 | 3.62 | 2.45 |
| 22:00 | 4219 | Sarmiento Resistencia vs CA 9 de Julio Rafaela | 1.84 | 3.11 | 4.28 |
| 22:00 | 4826 | Sportivo Penarol vs CD Argentino Monte Maiz | 3.31 | 3.16 | 2.08 |
| 23:00 | 1808 | Crucero Del Norte vs Juventud Antoniana | 1.80 | 2.95 | 4.40 |
| 23:00 | 3412 | Cuniburo FC vs Chacaritas FC | 1.95 | 3.10 | 3.55 |
| 23:15 | 3071 | Juan Aurich vs Alianza Universidad De Huanuco | 3.33 | 3.28 | 1.98 |
| 23:30 | 3728 | Los Chankas CYC vs Comerciantes FC | 1.32 | 4.55 | 7.69 |

### ALHAMISI - 14/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:30 | 5411 | Curico Unido vs O Higgins | 2.55 | 3.16 | 2.55 |
| 03:30 | 2642 | Internacional vs Sao Paulo | 2.08 | 3.14 | 3.33 |
| 03:30 | 4043 | Flamengo vs Atletico Pr | 1.74 | 3.54 | 4.13 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Septemba 13, 2023

Nipashe




Klopp atajwa ukocha Ujerumani UKURASA 22







Kushoto ni mashabiki wa Yanga, kulia wa Simba na katikati ni Naibu Waziri wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'MwanaFA', ambaye kwa niaba ya serikali, ametoa maagizo mazito kwa klabu hizo kuelekea michuano ya CAF. **PICHA: MAKTABA**

# Simba, Yanga zapewa maagizo mazito CAF

**Na Saada Akida**

## Serikali yatoa onyo kali ikikemea hujuma na kutaka umoja...

WAKATI Simba na Yanga zikijiandaa kwa michezo yao ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Power Dynamos ya Zambia na Al-Merrikh ya Sudan, serikali imetoa maagizo mazito ili kuhakikisha zote zinaiwakilisha vema nchi kwa kufika mbali kwenye michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

**Simba itashuka dimbani ugenini Jumamosi katika Uwanja wa Levy Mwanawasa, Zambia dhidi ya wenyeji wao Power Dynamos, ambako siku hiyo hiyo pia Yanga itakuwa nchini Rwanda kwenye Dimba la Pele mjini Kigali kuvaana na Al-Merrikh inayoutumia uwanja huo kutokana na kuwapo kwa machafuko ya kisiasa nchini kwao, Sudan.**

Kuelekea michezo hiyo na ile ya marudiano na endapo zote zitafuzu hatua ya makundi, serikali kwa kupitia Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA', amewataka viongozi wa klabu hizo kuwa wamoja katika kuhakikisha wanapeperusha vema Bendera ya Taifa Kimataifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwana FA alisema anaamini timu zote zimefanya maandalizi mazuri kujiandaa dhidi ya wapinzani wao hao na kuwatakia kheri katika mechi hiyo na kwamba wizara ina matarajio makubwa na klabu hizo kufanya vizuri katika michuano hiyo zaidi ya zilivyoyafanya msimu uliopita.

"Hiki ni kipindi cha kupeperusha Bendera ya Taifa, Simba na Yanga kuachana na maneno pamoja na kuhujumiana, yale mambo yetu tunayoyafanya kwenye ligi ya ndani tuyaweke pembeni na sasa tuungane na kushirikiana ili kuvuka katika hatua hii na kusonga mbele.

"Hatutaki kusikia maneno maneno au kufanyiana hujuma kama ilivyokuwa misimu ya nyuma, wote tunaenda kuwakilisha nchi mnatakiwa kusaidiana kwa sababu wote mnapeperusha Bendera ya Tanzania," alisema Mwana FA.

Aliongeza kuwa anaimani haitakuwa ngumu kama viongozi wa timu hizo wakiamua kushirikiana, lakini akaomba katika michuano hiyo wawe wamoja na kuona jinsi gani watafanya vizuri na kusonga mbele hadi fainali.

INAENDELEA UKURASA 23

# Robertinho atamba kupata dawa ya Power Dynamos

**Na Faustine Feliciane**

ZIKIWA zimebaki siku tatu kabla ya mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika raundi ya kwanza, Kocha wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema tayari ameandaa 'dawa' kwa ajili ya wapinzani wao, Power Dynamos na watawashangaza wakiwa nyumbani kwao.

Simba itakuwa mgeni wa Power Dynamos Jumamosi kwenye mchezo wa mkondo wa kwanza kusaka tiketi ya kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Robertinho alisema wapinzani wao hao wasitegemee kuiona Simba waliyocheza nayo kwenye tamasha la Simba Day Agosti 6, mwaka huu, kwani katika mchezo huo utakaochezwa Jumamosi wiki hii, wataingia uwanjani tofauti.

"Mchezo tuliokutana nao siku ya Simba Day ulikuwa na makusudio tofauti, huu wa Septemba 16, mwaka huu nao ni tofauti, huu ni mchezo wa maamuzi, nimetumia muda kuwasoma wapinzani wetu na tayari mikakati yangu imekaa sawa tunasubiri siku ya mchezo," alisema Robertinho.

Katika mchezo huo wa kirafiki ambao Power Dynamos walialikwa, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0, mabao ya Willy Onana na Fabrice Ngoma.

Alisema utofauti kwenye mchezo wa Jumamosi ijayo utaanzia aina ya wachezaji atakaochagua kuanza katika mchezo na aina ya mfumo atakaoutumia.

"Hautakuwa mchezo mwepesi kwa sababu wapinzani wetu nao wamejiandaa, lakini Simba ni timu kubwa yenye wachezaji wenye uwezo mkubwa na lazima tulionyeshe hili, tutatumia siku hizi chache zilizobaki kumalizia maandalizi yetu ambayo kwa kiasi kikubwa tumefika mbali, tunaomba tu sapoti ya mashabiki wetu,"

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >